**ANAYEDAIWA** kugonga na kusababisha vifo vya wafanyamazoezi sita atiwa mbaroni

UKURASA 3



**UTALII MPYA**
Sh. milioni tano mnyama anapewa jina ulipendalo

UKURASA 19


Nipashe
TESA
Jumanne Julai 25, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 12
NZUNDA NA BUBERWA
Wagunduzi wanaodhihirisha jinsi plastiki ilivyo mali

Ukurasa 13
Miradi ya kiuchumi ilivyofanikisha kufukuza tembo, kunufaisha jamii

Ukurasa 14
Hii ndiyo siri kisiwa cha maisha marefu

ELIMU
NA FAUSTINE FELICIANE, ALIYEKUWA MARA

**Ni kicheko wanaokwenda fomu 'V' mwezi ujao...**
•Watakapoanza ndani ya madarasa mapya 1,090 yaliyojengwa mikoa yote

KATIKA juhudi za kuandaa miundombinu ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha tano mwezi ujao, kampuni ya Twiga Mineral Cooperation, inawajenga vyumba vya madarasa zaidi ya 1,000 kwa nchi nzima.

Ujenzi huo, unaofanywa na kampuni ya kuchimba madini katika mgodi wa North Mara ya Barrick kwa kushirikiana na serikali, wawili hao wanamiliki kwa ubia kampuni ya Twiga Mineral Cooperation.

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow, anasema kwa pamoja watajenga madarasa 1,090 yatakayotumiwa na wanafunzi 49,000, kazi itakayofanywa katika shule 161.

Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) mapema Machi mwaka huu lilitangaza matokeo ya kidato cha nne na baadhi ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha tano wataanza masomo mwezi ujao.

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, anaongeza kuwa kwa ushirikiano na kwa pamoja kampuni hizo zimetoa dola za Marekani milioni 30 (zaidi ya Shilingi bilioni 73) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo mkubwa.

Anaongeza kuwa ujenzi wa vyumba vya madarasa unalenga kufanikisha programu maalum ya kusongesha mbele mustakabali wa shule (future forward

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow (katikati), akizungumzia faida za uzalishaji katika migodi ya Bulyanhuru na North Mara kwa ubia na serikali kupitia kampuni ya Twiga Mineral Corporation. Kulia ni Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa na Meneja wa Barrick Tanzania, Melkiory Ngido. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

kufanikisha shule kuchukua wanafunzi 49,000 wanaotarajiwa kuanza kidato cha tano mwaka huu. Tunaamini kuwa kujengwa vyumba hivi tutakuwa tumechangia juhudi za serikali katika kuinua elimu nchi nzima," anasema Dk. Bristow.

Halikadhalika, anaongeza kuwa kampuni hizo zimeweka

ana kuboresha miundombinu ya shule katika vijiji vinavyozunguka migodi yake ya North Mara na Bulyangulu uliopo Kahama mkoani Shinyanga.

"Tutaendelea kuboresha miundombinu ya shule kupitia programu hii lakini pia pale inapohitajika tunafanya hivyo katika vijiji vinavyozunguka migodi kwenye

anasema Dk. Bristow.

Anasema ushirika wa Barrick na kampuni ya Twiga mbali ya kujenga vyumba hivyo vya madarasa, pia wataendelea kuboresha miundombinu mingine kama barabara na huduma za maji safi na salama katika vijiji vinavyozunguka migodi yake.

elimu, tunaamini katika kwenye kuelimika ndipo vijana wanapoanza kutengeneza ndoto zao na kuzifikia," anasema Rais na Mtendaji Mkuu.

Anaungwa mkono na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, anayesema mkoa huo utaendelea kushirikiana na wawekezaji wakiwamo Barrick na kufanikisha miradi mbalimbali ya wananchi watakayoianzisha.

"Tunaunga mkono moja kwa moja mradi huu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa, hii ni kwa sababu inaenda kuongeza nguvu kwa jitihada za Rais Samia Samia Suluhu Hassan kuboresha elimu ya watoto wa Tanzania," anasema Mtanda.

"Kazi yetu ni kusimamia maendeleo ndani ya mkoa, tutafanya hivyo na kuimarisha mahusiano mema kati ya wawekezaji na wananchi, lakini pia tunaunga mkono miradi yote ambayo ina faida kwa wananchi na serikali," anasema Mtanda.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu katika elimu anaeleza kuwa imevisaidia vijiji vinavyozunguka mgodi wa North Mara kwa kujengewa madarasa na miundombinu mingine.

"Tukipewa miradi kama hii ambayo inagusa moja kwa moja jamii yetu, mfano ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na vifaa mashuleni ni miradi ambayo inakwenda kunufaisha jamii moja kwa moja, lakini inaisaidia na kufanikisha juhudi za serikali za kuwafikia wananchi na kuwapa huduma muhimu," anasema Mtanga.

Anasema kwa Wilaya ya Tarime Vijijini unapopatikana mgodi wa North Mara vijiji vya Nyangoto, Nyabichune, Mjini Kati pamoja na Matongo vimenufaika na miradi hiyo ya Barrick.

Anasema zipo shule zilizojengwa katika vijiji hivyo na kuboresha miundo mbinu yake na kushukuru uwekezaji huo ambao unasaidia Watanzania


UKURASA 11

**Nipashe**
Jumanne Julai 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581382
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

RIPOTI MAALUM

# Kila saa kuna timbwili katika ndoa 13 nchini

**NDANI** ya miezi 10 watoto 18,000 wamekosa malezi kisa wazazi kuachana, wataalamu wafichua mizizi 19 ya tatizo... *Endelea Uk. 4*




UKURASA WA 7

## WANYAMAPORI WAUA WATU 1,000 NCHINI

JUMLA ya watu 1,069 wamepoteza maisha, 642 kujeruhiwa na wanyamapori kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi 2019...



UKURASA WA 15

## WAZIRI AWASHUKIA ASKARI MGAMBO WANAOPOKA BIDHAA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amewataka askari mgambo wa Jiji hilo kutotumia nguvu na mabavu kwa kuwanyang'anya...

UKURASA WA 19

## MFUGAJI AIBUKA MSHINDI BAJAJI KAMPENI YA CRDB

KATIKA Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Joshua Loketa, amesimama huku akitabasamu akiwa ameshikilia funguo za bajaji yake mpya...

## Kinana: Msibadili viongozi kama mashati



UKURASA 2

## Vifaa vya mawasiliano vyafungwa, zimo laini za 'tuma kwa namba hii'

UKURASA 2

**MICHEZO** KIBU AIPA SIMBA SARE UTURUKI, SAKHO AUZWA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Vifaa vya mawasiliano vyafungwa, zimo laini za 'tuma kwa namba hii'

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema katika kipindi cha mwaka mmoja, imefungia vifaa vya mawasiliano pamoja na simu 108,395 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuhusika na uhalifu, ulaghai, vitendo vya udanganyifu na wizi.

Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Dk. Jabiri Bakari, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu taarifa ya maendeleo ya usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano nchini kwa mwaka 2022/23.

Dk. Jabiri alisema TCRA imeendelea kubaini simu za ulaghai zinazoingia nchini na hatua stahiki zimekuwa zinachukuliwa.

"Kutokana na hatua hiyo, idadi ya simu za udanganyifu imeendelea kupungua kuanzia mwaka 2020 hadi Juni 2023. Mwaka jana, Septemba, tulibaini matukio machache ya simu za ulaghai," alisema Dk. Jabiri.

Kuhusu usimamizi wa simu za ndani na kimataifa, alisema idadi ya dakika za simu za kimataifa zinazoingia nchini zimepungua kutoka dakika 3,136,692 Julai mwaka jana, hadi kufikia dakika 2,900,165 Juni mwaka huu, sawa na asilimia 7.54. Pia, alisema idadi ya dakika za simu za kimataifa zinazotoka nchini zimepungua kutoka dakika 2,405,522 Julai mwaka jana hadi kufikia dakika 2,226,071 Juni mwaka huu, sawa na asilimia 7.46.

"Kupungua kwa simu za kimataifa kunasababishwa na mabadiliko ya teknolojia na upatikanaji wa uchaguzi mbadala wa kupiga simu kupitia mitandao ya intaneti kama vile WhatsApp, Facebook, Telegram, Zoom na kadhalika," alisema Dk. Jabiri.

Alibainisha kuwa idadi ya dakika za simu za kitaifa ndani ya mtandao mmoja zimeongezeka kutoka dakika 6,172,696,579 Julai mwaka jana hadi dakika 7,012,574,045 Juni mwaka huu sawa na asilimia 13.61.

Alisema idadi ya dakika za simu za kitaifa nje ya mtandao mmoja zimeongezeka kutoka dakika 4,879,102,325 Julai mwaka jana hadi kufikia dakika 5,064,800,480 kufikia Juni mwaka huu sawa na asilimia 3.81. Dk. Jabir alisema ongezeko la simu za kitaifa linasababishwa na ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua Barabara ya Maliki inayounganisha Barabara ya Umoja wa Mataifa na Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila.
**PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Rais Samia kuzindua Mnara wa Mashujaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Mnara wa Mashujaa katika Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma, ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa eneo hilo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana kuhusu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mashujaa inayofanyika kila mwaka Julai 25.

Waziri Jenista alisema maadhimisho hayo yatafanyika katika mikoa na wilaya zote nchini kwa kufanya shughuli za kijamii ikiwamo kupanda miti, kufanya usafi maeneo ya kijamii na kufanya kumbukumbu ya mashujaa kwa mikoa na wilaya ambayo ina minara au makaburi ya mashujaa hao.

Mbali na hayo, Waziri Jenista alibainisha kuwa shughuli za maadhimisho hayo ni pamoja na gwaride la maombolezo, uwekaji wa silaha za asili na maua kwenye Mnara wa Mashujaa pamoja na dua na sala kutoka kwa viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini nchini.

Alisema ujenzi wa Mnara na Uwanja wa Mashujaa umekamilika kwa hatua ya kwanza kwa kujenga Uwanja wa Mashujaa utakaokuwa unatumika kwa gwaride la vyombo vya ulinzi na usalama na matukio na shughuli zingine za serikali.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Innocent Bashungwa, aliipongeza serikali kwa uamuzi wa ujenzi wa mnara huo na kuahidi wizara hiyo itatoa ushirikiano katika hatua zote za ujenzi hadi kukamilika kwake.

# Kinana: Msibadilishe viongozi kama mashati

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amesema hakuna sababu ya wananchi kubadilisha viongozi kama mashati kwa kuwa kunarudisha nyuma maendeleo.

Akizungumza wilayani Kondoa, mkoani Dodoma wakati wa mkutano wa hadhara uliondaliwa na Mbunge wa Jimbo la Kondoa, Dk. Ashatu Kijaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Kinana alizungumzia umuhimu wa wananchi kujenga tabia ya kutobadilisha viongozi wao kama mashati kama hakuna ulazima wa kufanya hivyo.

Alisema kila binadamu ana kasoro, hakuna mkamilifu, lakini wananchi hususan wapigakura wasimwadhibu mtu kwa mambo madogo, badala yake waangalie mambo makubwa na mazuri anayoyafanya huku akitoa mfano kuwa majimbo yote ambayo wabunge wake hawabadilishwi kama mashati hupiga hatua kubwa za maendeleo.

"Ilani yetu ya uchaguzi ina kurasa 303, lakini kitabu hiki (kinachoonyesha utekelezaji wa Ilani) katika Jimbo la Kondoa kwa kipindi cha miaka miwili na nusu, kuna kurasa 100 zinazoelezea Jimbo la Kondoa Vijijini mambo ambayo yamefanyika. Ni kweli serikali imefanya makubwa, vile vile kuna mtu ambaye ni kiungo kati ya serikali kuu, Halmashauri, Chama Cha Mapinduzi na Bunge naye ni mbunge," alisema.

Alifafanua kuwa inawezekana mbunge asifanye kila kitu ni binadamu na anaweza kuwa na kasoro, lakini mtu akitaka kuishi na mwenzake vizuri atafute mema yake asitafute upungufu wake.

"Wote tunavyoishi ukitafuta upungufu wa mtu mtakosana ukizungumza mema yake mtaishi pamoja kila binadamu ana upungufu wake hata mimi nina yangu. Na yeye atakuwa anajua upungufu wao, lakini yote yanawekwa kando na kutafuta mema na kufanya maisha kuwa mazuri," alisema.

Aidha, alisisitiza katika kufanikisha maendeleo yoyote ni lazima kuwapo umoja na mshikamano, kwa kuwa mambo hayo yasipokuwapo maendeleo yatakuwa hafifu kwa sababu viongozi na wananchi watakuwa wakibishana katika kila jambo.

"Mnataka kuweka mradi wa maji mnabishania mradi uende wapi, mnataka kujenga shule mnasema ijengwe wapi, mnabishana hadi fedha zinarudi serikali kuu. Mnataka kuamua nyumba za walimu zijengwe wapi hamkubaliani. Mkiwa na umoja maendeleo yatakuwa ya haraka zaidi.

"Mkitaka kuamua fedha tulizonazo za ujenzi wa barabara ni ndogo tuanze na barabara ipi mkavutana mtaendelea kubishana hadi hapo fedha zitakapokuwa zimerudi serikali kuu. Kila ifikapo Juni serikali inatafuta fedha zote ambazo hazikutumika zinarudishwa katika hazina kuu ya serikali, niliwahi kuwa mbunge na hilo nalijua.

"Kwa hiyo hakikisheni kila fedha iliyotengwa zinatumika kwa yale yaliyokusudiwa lakini vile vile kwa miradi iliyokusudiwa.

"Ni vema ikafahamika kuwa kiongozi hawezi kufanya kazi wala kuleta maendeleo peke yake bali na wananchi wote kwa ujumla wao," alisema.

# Aliyedaiwa kugonga, kuua wafanyamazoezi akamatwa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limemkamata dereva wa gari lenye namba za usajili T 476 DZL, Toyota Hilux, Oswald Kaijage (39), anayedaiwa kuwagonga na kusababisha vifo vya watu sita waliokuwa wanafanya mazoezi katika eneo la Sabasaba wilayani Ilemela.

Oswad anadaiwa kuwa baada ya kusababisha vifo vya watu hao na kujeruhi 16, alitoroka. Jeshi la Polisi lilianza kumtafuta.

Jijini hapa jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, ACP Wilbord Mutafungwa alithibitisha kukamatwa kwa dereva huyo katika Kata ya Kisesa wilayani Magu.

Kamanda Mutafungwa alisema watu waliogongwa ni kikundi kinachoundwa na wafanyakazi wa Hoteli ya Adden Palace, wateja na majirani wa hoteli hiyo ambao huwa wanafanya mazoezi hayo kila Jumamosi.

"Tumefanikiwa kumkamata Oswald kufuatia msako mkali. Baada ya tukio hilo, alikwenda kulitelekeza gari hilo katika kituo cha mafuta kisha kutokomea kusikojulika," alisema.

Kamanda Mutafungwa alitaja majina ya waliofariki dunia katika ajali hiyo ni Peter Fredrick, Shadrack Safari, Celestine Daud, Hamisi Waziri, Aman Matinde na Makolongo Manyanda.

Aliwataja majeruhi ni Magnus Masanja (26) ambaye ni mkazi wa Isamilo, Godfrey Benard (25-30), Remidius Pontian (24), Grace Dickson (30) ambaye ni mkazi wa Iloganzala, Husein Hassan (20) na Baraka Jeremiah.

Alisema majeruhi saba wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Sekou Toure), huku wengine wanane wakipatiwa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando kwa uangalizi maalum na wengine wamepatiwa matibabu na kuruhusiwa.

Kamanda Mutafungwa alisema uchunguzi wa awali umefanyika. Upelelezi ukikamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Alivitaka vikundi vyote vya mazoezi kujisajiri katika ofisi za utamaduni ngazi za wilaya, mamispaa na jiji na kupewa miongozo na maelekezo ya namna bora ya kufanya mazoezi kwa kuzingatia sheria na taratibu.

Vilevile, alivitaka vikundi hivyo kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi katika wilaya husika endapo watahitaji kutumia barabara wakati wa mazoezi yao ili wapewe ulinzi wa kusimamia usalama wao kupitia askari wa usalama barabarani.

Kamanda Mutafungwa pia aliwataka waendeshaji vyombo vya moto kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani.

# Benki yajenga vyoo shuleni

**Na Mary Geofrey,** ROMBO

WANAFUNZI 700 wa Shule ya Msingi Kikelelwa wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro, wameondokana na adha ya kutumia matundu machache baada ya Benki ya Taifa ya Biashara (TCB) kujenga matundu ya vyoo 18 shuleni huko.

Mkurugenzi wa Hazina wa TCB, Wenceslaus Fungamtama, akizindua matundu hayo kwa niaba ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema juzi kuwa lengo la kujenga vyoo hivyo ni kuboresha mazingira na utulivu wa kujifunza kwa wanafunzi hao wawapo shuleni.

"Ili kuunga jitihada za serikali za kuboresha huduma za kijamii ikiwamo afya na elimu, Benki ya TCB hutenga Sh. milioni 300 kila mwaka, kwa mwaka huu zimetumika kujenga madarasa, nyumba za walimu na vyoo katika maeneo mbalimbali nchini," alisema Fungamtama. Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Charles Amos, alisema kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo, wanafunzi walilazimika kupanga foleni kusubiriana huku wale wadogo wakijikojolea.

"Tuna watoto waliokuwa wanatoroka kwenda nyumbani kwa aibu ya kujikojolea, hasa muda wa mapumziko ambao wanatoka darasani kwa pamoja, lakini sasa kwa vyoo hivi ni wazi kutakuwa na utulivu wa kujifunza," alifafanua Amos.

Dada Mkuu wa shule hiyo, Careen Jonas, alisema vyoo hivyo vimejengwa kisasa, vikizingatia miundombinu ya wenye ulemavu, pia vina chumba maalum cha kubadilishia taulo kwa wasichana.

Ofisa Elimu Idara ya Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Alice Makule, alisema hivi sasa shule ina wanafunzi 768, wavulana 385 na wasichana 378 ambapo kwa uwiano ilitakiwa kuwe na matundu 16 kwa wavulana na 19 kwa wasichana.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza tundu moja la choo kutumiwa na uwiano wa wanafunzi 20 wa kike au 25 wa kiume.

Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Machi 2017, ilibainisha hali mbaya ya miundombinu na samani katika shule za serikali huku kukiwa na hali nzuri kwa upande wa shule zinazomilikiwa na watu na taasisi binafsi.

# Wamiliki wa maghala wasema mafuta yapo

**Na Elizabeth Zaya**

WAMILIKI wa maghala ya mafuta wameihakikishia serikali hakuna uhaba wa mafuta nchini na kuahidi kuyasambaza katika maeneo yote yenye uhitaji nchini.

Ni ahadi waliyoitoa juzi kwa Waziri wa Nishati, January Makamba aliyeambatana na Kamishna wa Mafuta na Gesi Asilia, Michael Mjinja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andilile, katika ziara ya kukagua baadhi ya maghala ya kuhifadhi mafuta mkoani Dar es Salaam.

Viongozi hao walifanya ziara hiyo kujiridhisha na mwenendo wa upatikanaji wa nishati hiyo nchini.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Meru Petroleum, Charles Maingu, alisema ndani ya siku 10 zilizopita, walitoa mzigo wa mafuta wa lita milioni 28 yaliyosafirisha ndani ya nchi na nje ya nchi, na kwamba mzigo mwingine wenye dizeli lita milioni 27, petroli lita milioni 40 watapokea mwezi ujao.

"Pia mzigo wa Septemba mafuta ya petroli ni lita milioni 19.5 na dizeli lita milioni 18. Nisema tu kwamba hakuna changamoto ya mafuta, yapo ya kutosha," alisema Maingu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy, Fatma Abdallah, alisema kuwa mwezi huu kumekuwa na mahitaji makubwa ya mafuta tofauti na mwaka jana na kwamba hadi juzi, walikuwa wameuza petroli na dizeli lita zaidi ya milioni 36.

"Tunatarajia kuuza zaidi ya lita milioni 50 za mafuta hadi mwezi huu mwishoni. Tunauza mafuta yetu kwa wateja wakubwa wadogo, meli zinazokuja pia zina mzigo wetu na kabla ya Julai haijaisha tunatarajia kupata lita milioni 16," alisema Fatma na kuongeza:

"Lakini Agosti tutapata mafuta ya dizeli na petroli lita zaidi ya milioni 60, niwatoe hofu wauzaji wakubwa na wadogo mafuta yapo ya kutosha na tunashirikiana kwa ukaribu na serikali."


Lindi Jumbo Limited
TANZANIA

Lindi Jumbo
Limited

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF LOGISTICS, WAREHOUSING AND SHIPPING SERVICES**
**REFERENCE NO LJL-2023-004 LINDI JUMBO GRAPHITE PROJECT**

**LINDI JUMBO Limited ("the Company")** is a Tanzanian registered exploration and mining company, currently developing the Lindi Jumbo Graphite Mine in the Ruangwa District in south-eastern Tanzania. The mine is currently in construction and estimated to be completed in Q4 2023, with production anticipated to commence in January 2024. The mine has access to existing logistics infrastructure, including optionality to export Lindi Jumbo product through the port of Mtwara (200km) and the port of Dar Es Salaam (460km).

The Company invites experienced and reputable companies to express their interest in providing local logistics, warehousing and associated shipping and freight forwarding services to the Lindi Jumbo Mine.

**SCOPE OF SERVICE (BRIEF DESCRIPTION)**

The Company has a bagging facility and product warehouse on site from where the product will be collected and transported to the Port of Mtwara and or Dar es Salaam (or otherwise agreed upon) for export purposes. The use of an intermediate warehouse, with sufficient capacity will be required prior to exporting.

The Scope of Work shall include but not limited to the following:

- **Local Logistics Services:** The Selected Bidder shall provide local road logistics support for all aspects of the supply chain, which will include transporting the product from the mine warehouse to an interim warehouse and from the warehouse to the preferred and agreed upon export port.
- **Warehouse Management:** The Selected Bidder shall be responsible for the management of the warehouse/s, whether it/they are self-owned or leased. All aspects of warehouse management including product receipt and issuing, proper storage, inventory control, loading of the product for transportation, containerizing, unloading of the product, etc. Critical to warehousing is the capacity to store sufficient volumes in a secure and controlled environment. Product will have to be moved from the mine daily due to limited storage capacity at the mine warehouse.
- **Freight Forwarding and Shipping Agency Services:** The Selected Bidder shall be responsible for managing the administrative and operational process for exporting the product from the agreed upon port/s in Tanzania. This will include vessel bookings in line with the Company's sales book.
- **Inventory Management System**: The Selected Bidder shall utilize an inventory management and integrated document system throughout the supply chain process for administrating movement of stocks. The IMS system must allow for a real-time dashboard available to the Company. The IMS system must include barcoding / QR coding equipment that can be established at the mine warehouse and be used by the mine warehousing team.

Companies or organisations expressing their interest are invited to document their request with:

1. Proof of registration with the Tanzania Revenue Authority (TRA).
2. Company Information - including but not limited to corporate details, trading name, company registration number, Local Content Compliance, Tax Clearance Certificate for the latest year.
3. Capability Statement.
4. Copy of certificates of accreditation with other operations.
5. List of Insurances, where applicable.
6. Supply Chain Model/s that would best suit the Lindi Jumbo Mine and breakdown of the indicative cost – taking note that the annual volumes to be moved once plant reaches steady state will be approximately 40'000tonnes per annum. Initial volumes from Jan-June 2024 will be approximately 500, 1000, 1500, 2000, 2500 and 3000tonnes per month respectively; from July onwards, volumes will be between 3500 and 4000tonnes per month.
7. Specify details and quantity of the infrastructure, vehicles and equipment that is owned by the organization and availability of such to provide the service to the Lindi Jumbo Mine.
8. Specify details of the Inventory Management System that is employed by the organization that will be used to service Lindi Jumbo.

Companies which have the ability, capacity and resources to implement the services listed above should express their interest by sending together with the documents stated in the above section through an email to info@lj.co.tz (Max email size 20 MBs), all documents must be submitted in English Language on or before 24:00hrs East African Time (EAT) on 07-August-2023. The subject of the email should be **"EOI LJL-2023-004-COMPANY NAME".**

Lindi Jumbo Limited will review and assess the documents provided by companies that have expressed interest in accordance with this EOI and conduct evaluations based on internal criteria to determine which companies will be included in the list of pre-qualified companies. Only the pre-qualified companies will receive, by signing a Non-Disclosure Agreement (NDA), an invitation to bid as a continuation of the call for tender process.

Lindi Jumbo Limited is not bound to accept the lowest or any tender offer received, and the adjudication of the tender will be based solely on the discretion of the company with consideration given to both qualification and commercial aspects.

**Lindi Jumbo Limited (Company No. 124563)**
**Cape Town Fish Market, 3rd floor, Plot No. 180, Msasani Village Block "B" P.O. Box 33773, Dar es Salaam Tanzania**
**Email: info@lj.co.tz Web: www.lindijumbo.co.tz**

MAKALA MAALUM

# Kila saa kuna timbwili katika ndoa 13 nchini

## -Miezi 10 tu watoto 18,000 wamekosa malezi, wataalamu wafichua mizizi 19 ya tatizo...

Na Jenifer Gilla

MIGOGORO 28,773 ya ndoa imefikishwa mbele ya Maofisa Ustawi wa Tanzania Bara. Watoto 18,922 wameathirika kutokana na migogoro hiyo, serikali imethibitsha.

Shida ni nini? Wasaikolojia tiba na wasuluhishi wa migogoro ya ndoa wametaja mambo 19 yanayochangia migogoro hiyo, sasa kukishuhudiwa ongezeko kubwa la talaka nchini.

Wadau hao wa masuala ya ndoa na familia wamemtajia mwandishi wa habari hizi mambo 19 yanayosababisha migogoro katika ndoa inayochangia ongezeko linaloshuhudiwa la talaka nchini.

Mambo hayo ni pamoja na: Kukosekana stadi nzuri za mawasiliano; uvumilivu; kutegemea ndugu na majirani kutatua migogoro hiyo badala ya wataalamu; hali ya kipato; wanandoa kutofahamu wajibu wao; kutohusisha viongozi wa dini; na kutokuwa wakweli, hasa wakati wa uchumba.

Mengine yanajumuisha: Mila na desturi zisizofaa; udhaifu wa malezi kwa watoto; taarifa zisizokuwa na uthibitisho; kushindwa kukubaliana katika mambo yahusuyo familia; mwenza mmoja kuhisi kupingwa mawazo yake na mweziwe; na hisia kali dhidi ya mwenza.

Vilevile, lawama, tuhuma na kutoridhika; upweke kutokana na majukumu ya kikazi; tofauti kubwa ya elimu na kipato; na kutokuwa, maandalizi bora wakati mtu anapoamua kuingia katika ndoa, kushindwa kutoa mahitaji ya kimwili kwa mwenza kama inavyotakiwa na wanandoa kutosameheana hasa kwa vitu vidogo.

Ni hoja zinazoanikwa na wadau hao ikiwa ni wiki moja tangu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, kubainisha Jumatatu ya jumla lililopita kuwa kati ya Julai 2022 na Aprili mwaka huu, serikali imepokea migogoro 28,773 ya wanandoa.

Takwimu hizo za serikali zinatoa ishara ya kuwapo wastani wa migogoro ya ndoa 106 kila siku sawa na migogoro 13 kwa kila saa ya kazi.

Ni takwimu ambazo Waziri Dorothy alizitaja alipofungua kongamano la kwanza la kutafuta suluhisho la kukithiri kwa talaka nchini, akibainisha kuwa kati ya migogoro hiyo 28,773, migogoro 22,844 ilipatiwa suluhu, huku 5,929 ikipelekwa ngazi inayofuata ya mahakama.

Dk. Dorothy alisema migogoro hiyo imechangia watoto 18,922 kuathirika katika malezi, baadhi wakikimbilia mitaani, kuingia katika matumizi ya dawa za kulevya au/na ndoa za utotoni.



Waziri alizitaja sababu za kuongezeka migogoro hiyo kuwa ni pamoja na mawasiliano hafifu ya wanandoa, hali ya kipato, wanandoa kutofahamu wajibu wao, mila na desturi zisizofaa, udhaifu wa malezi kwa watoto na kufanya uamuzi baada ya kupewa taarifa zisizokuwa na uthibitisho.

Msaikolojia Tiba, Dk. Saldeen Kimangale, anayefanya kazi katika Kituo cha Afya Somedics mkoani Dar es Salaam, anasema sababu kuu ya wanandoa kukwaruzana ni kukosa stadi nzuri za mawasiliano na kutojifunza ustahimilivu.

"Hata pale panapotajwa kuwa kukosa uaminifu ndiyo sababu ya migogoro na talaka. Ukweli ni kuwa pakiwa na mawasiliano mazuri, yenye kuleta maana, mgogoro huo utatuliwa na maisha yakaendelea vizuri tu," anasema.

Dk. anataja sababu zingine ni kushindwa kukubaliana katika mambo yanahusu familia, mwenza mmoja kuhisi kupingwa mawazo yake na mweziwe, kuwa na hisia kali (mapenzi yaliyopitiliza) dhidi ya mwenza, lawama, tuhuma na kutoridhika, upweke kutokana na majukumu ya kikazi na tofauti kubwa ya elimu na kipato baina ya wanandoa.

Mtaalamu wa Maendeleo na Ushauri wa Kijamii, James Mlali, anasema migogoro katika ndoa inachangiwa na kutokuwa na maandalizi bora wakati mtu anapoamua kuingia katika maisha ya ndoa - vijana wengi huingia katika hatua hiyo muhimu kwa kufuata mkumbo, mihemko na maslahi ya kibiashara.

Anasema wazazi wengi wanakwepa jukumu la kuwaelimisha vijana wao mambo ya msingi ya kuzingatia wanapojiandaa kuingia katika ndoa, hivyo kuchangia kuwapo migogoro hiyo - wengi wakijikuta wanaingia kwa kufuata mkumbo, tamaa za mwili na maslahi ya kibiashara.

"Kijana huyu sasa akishaingia katika ndoa, akagundua yale aliyokuwa nayo kichwani siyo uhalisia uliopo, majukumu anayokutana nayo hakuwa amejipanga na kujiandaa nayo, matokeo yake anatafuta mlango wa kutokea," Mlali.

Sababu nyingine kwa mujibu wa Mlali ni kushindwa kuweka usawa kati ya kazi na familia, kipato kisishotosheleza na kushindwa kutoa mahitaji ya kimwili kwa mwenza kama inavyotakiwa.

Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi kinachotoa msaada wa kisheria na ushauri nasaha hasa kwa wanawake na watoto kilichoko Sinza wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Gladness Munuo, anasema migogoro mingi ya ndoa husababishwa na kutosameheana katika vitu vidogo.

Gladness, mwenye uzoefu wa miaka 10 katika kusuluhisha migogoro ya ndoa, anataja jambo lingine linalochochea migogoro hiyo ni wanandoa kufunga ndoa pasi na kujuana kwa muda mrefu na kutokuwa wakweli wanapoingia katika uhusiano huo.

"Ukweli ndiyo msingi wa maelewano. Weka wazi kama ulishakuwa na ndoa nyingine kabla ya hii, kama una mtoto. Kukiwa na uwazi, maisha yanakwenda vizuri," anasema Gladness.

Zainab Mselemo, mkazi wa Kinyerezi jijini Dar es Salaam, anasema kilichomfanya adumu katika ndoa kwa miaka 20 sasa ni uvumilivu, kujishusha na kushirikisha viongozi wa dini pale anapopitia changamoto katika ndoa yake.

Alisema mwanzoni alikuwa akipeleka mashtaka kwa ndugu zake na kukikuta badala ya kutatua tatizo, mgogoro ulikuzwa zaidi, hata kufikia hatua kaka zake walimpiga mumewe kwa madai ya kuumizwa na vitendo vyake dhidi ya dada yao. Ni hatua iliyosababisha watengane kwa miezi mitatu.

"Nilijifunza kupitia mgogoro huo kwa sababu baada ya hapo mume wangu alikwenda kunishtaki kwa shekhe ambaye alituita na kutusuluhisha, ndipo nikaona tofauti ya kiongozi wa dini na ndugu na jamaa katika usuluhuhi wa ndoa," Zainab anawasilisha uzoefu wake wa milongo miwili katika ndoa.

### NINI KIFANYIKE

Mwandishi anaporejea kwa Dk. Saldeen kujua mbinu za kukabiliana na migogoro hiyo, mtaalamu huyo anashauri jamii ifundishwe stadi bora za kuwasiliana katika ndoa, ili kujenga misingi ya kuelewana - yenye kulenga kutafuta suluhisho la pamoja na siyo ushindani.

Vilevile, anashauri wanandoa wawe na mawazo chanya kwa wenzi wao. Wanapaswa kufahamu kuwa kukosea ni jambo la kawaida. Wapeane muda wa kurekebisha pale wanapokwenda kinyume cha matarajio yao.

"Linalohusu familia tupange pamoja, tuache ubinafsi. Tusipende kuwashirikisha watu wa nje hata kama ni kaka zetu au dada zetu, kwani ninyi mtapatana, lakini mliowashirikisha wataendelea kuwatafsiri kwa kutegemea taarifa mlizowapa," anasema Dk. Saldeen.

Msaikolojia Tiba huyo pia anasema kunatakiwa kuwekwa msingi mzuri katika mafundisho ya ndoa kuanzia ngazi ya familia, ili kuwawekea misingi mizuri vijana kuhusu mambo muhimu wanayotakiwa kuzingatia wanapoingia katika ndoa.

Anasema wazazi wanalo jukumu kuwafundisha vijana wao vigezo muhimu vya kuzingatia wakati wanatafuta wenza, muda sahihi wa kuchumbia na umuhimu wa kumshirikisha Mungu wakati wanapitia hatua zote hizo hadi kufikia kufunga ndoa.

"Kijana asipopata elimu hii, ataingia katika ndoa kwa pupa, kisa tu afanye harusi kubwa au mwenza aliyempata ana kipato kizuri. Unakuta vijana wamechumbiana miezi miwili tu hata hawajajuana vizuri wanakwenda kuoana. Baadaye tabia zilizojificha zikionekana, migogoro inaanza na ndoa kuvunjika," anafafanua.

Anashauri semina za ndoa ziongezwe kanisani, misikitini na wakati wa mafunzo ya ujasiriamali ili kuwapatia mafundisho sahihi wanandoa na vijana wanaotarajia kuingia katika maisha ya ndoa. Yatawasaidia kudumu katika ndoa zao.

"Walio katika ndoa ni vizuri kuangalia namna nzuri ya kutatua migogoro kuliko kuvunja uhusiano, kwa sababu katika kuvunja uhusiano kuna hasara nyingi kwao na hata watu wanaowazunguka ikiwamo watoto," anashauri.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi kinachotoa msaada wa kisheria na ushauri nasaha, Gladness, anashauri kurudisha mila na desturi za kuwafunda vijana kuhusu ndoa kama ilivyokuwa zamani.

Gladness anasema anaamini mila na desturi hizo ni fursa muhimu kwa vijana kupewa misingi na elimu itakayowasaidia wanapokuwa katika ndoa.

### HALI YA NDOA

Ripoti ya Utafiti wa Ufuatiliaji wa Kaya (NPS) ya mwaka 2021 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), inabainisha kuwa asilimia 57 ya Watanzania hawako katika ndoa.

Utafiti huo ulibaini wakazi wa mijini, wengi hawako katika ndoa kulinganishwa na wa vijijini. Idadi ya wasioishi katika ndoa vijijini ni asilimia 55.5 ya waliofikia umri wa kuoa na kuolewa, huku mijini ni asilimia 61.5 sawa na tofauti ya asilimia sita.

Ripoti hiyo ya NBS inaonyesha mgawanyo wa wasio katika ndoa ni: Wanandoa waliotengana (asilimia tano); waliopeana talaka (asilimia 1.9), wasiowahi kuwa katika ndoa (asilimia 38.9), wajane na wagane (asilimia 5.4) na wanaoishi kiuchumba (asilimia 6.1).

## TANGAZO

# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30/06/2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo mwaka ya 30.06.2023 | Robo mwaka ya 31.03.2023 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha tasilimu | 1,752 | 1,891 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 2,875 | 3,173 |
| 3 | Uwekezaji katika amana serekalini | 0 | 0 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 5,396 | 6,625 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushuhulikiwa | 201 | 204 |
| 6 | Miamala baina ya matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili zililizo afikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za wateja zilizo kubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 35,718 | 32,631 |
| 12 | Mali nyingine | 2,738 | 2,298 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | 35 | 35 |
| 14 | Akauti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali zisizohamishika , mitambo na vifaa | 1,574 | 1,612 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 50,289 | 48,469 |
| | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za wateja | 36,471 | 35,265 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha tasilimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko za kodi na gharama zitakazolipwa | 239 | 146 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala isiyoshuhulikiwa baina ya matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 0 | 0 |
| 27 | Dhima nyingine | 515 | 430 |
| 28 | Madeni | 555 | 555 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **37,780** | **36,396** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 29)** | **12,509** | **12,073** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 10,227 | 10,219 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | 805 | 765 |
| 34 | Faida (hasara) ya kipindi husika | 765 | 377 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 712 | 712 |
| 36 | Stahiki ya mwenye hisa chache | 0 | 0 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **12,509** | **12,073** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | **3,584** | **2,352** |
| 39 | Mikopo chechefu | 1,808 | 2,448 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 722 | 834 |
| 41 | Malinyingine chechefu | 0 | 0 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 24.87% | 24.91% |
| | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 4.95% | 7.48% |
| | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 98.42% | 93.36% |
| | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 71.03% | 67.32% |
| | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 81.76% | 80.99% |
| | Ongezeko la amana | 3.42% | 0.97% |
| | Ongezeko la mali | 3.75% | 0.60% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA MWAKA UNAOISHIA 30/06/2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka wa sasa 30.06.2023 | Robo ya Mwaka Linganishi 30.06.2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30.06.2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mapato ya riba** | **1,552** | **1398** | **3,107** | **2,885** |
| 2 | Gharama za riba | 426 | 391 | 783 | 814 |
| 3 | Madeni viza yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **1,067** | **1,007** | **2,240** | **2,071** |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 59 | 0 | 84 | 0 |
| 6 | **Mapato yasiyo na riba** | **346** | **222** | **717** | **499** |
| | 6.1 Faida /hasara zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 18 | 11 | 52 | 30 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 317 | 204 | 625 | 413 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato mengine | 11 | 7 | 40 | 56 |
| 7 | **Gharama zisizo za riba** | **1,113** | **1,077** | **2,227** | **2,054** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | 542 | 540 | 1,087 | 1060 |
| | 7.2 Ada na kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine za uendeshaji | 571 | 537 | 1,140 | 994 |
| 8 | **Faida/(hasara) ya uendeshaji** | **300** | **152** | **730** | **516** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | 114 | 45 | 168 | 90 |
| 10 | **Faida/(hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **186** | **107** | **562** | **426** |
| 11 | Mapato mengine yaliojumuishwa (bainisha) | 202 | 0 | 203 | 0 |
| 12 | **Jumla ya faida /(hasara) iliojumuishwa kwa mwaka** | **388** | **107** | **765** | **426** |
| 13 | idadi ya waajiriwa | 49 | 49 | 49 | 49 |
| 14 | mapato kwa hisa | 3.79% | 1.05% | 7.48% | 4.19% |
| 15 | idadi ya matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAHADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa mali | 0.38% | 0.23% | 1.55% | 0.92% |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa fedha za wanahisa | 1.51% | 0.98% | 4.57% | 3.89% |
| | uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 58.64% | 66.48% | 58.24% | 60.70% |
| | uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani ya mali zinazozalishwa | 3.12% | 3.20% | 6.55% | 6.95% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30/06/2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uendeshaji | Robo ya mwaka ya sasa 30.06.2023 | Robo ya Mwaka 30.03.2023 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30.06.2023 | Limbikizo la mwaka Linganishi 30.06.2022 |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato/(hasara) halisi** | **300** | **429** | **730** | **516** |
| **Marekebisho kwa ajili ya:-** | - | - | - | - |
| Uchakavu | 100 | 63 | 232 | 120 |
| **Badiliko halisi katika mikopo** | **(3,087)** | **(170)** | **(3,961)** | **(759)** |
| Faida / (hasara) kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika amana | 1,206 | 340 | 3,295 | 3,277 |
| Mabadiliko katika amana za muda mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 178 | (160) | (381) | 649 |
| Mabadiliko halisi katika mali nyingine | (440) | (335) | (757) | 28 |
| Kodi iliyopitwa | (114) | (54) | (168) | (90) |
| Mengineyo (bainisha) | 202 | 1 | 203 | (604) |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uendeshaji** | **(1,655)** | **114** | **(807)** | **3,137** |
| | | | | |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uwekezaji** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa mali za kudumu | (22) | - | (421) | (409) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa amana zisizoshuhulikiwa mawakala | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshuhulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (15) |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uwekezaji** | **(22)** | **-** | **(421)** | **(424)** |
| | | | | |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za kifedha** | | | | |
| Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Ongezeko la hisa | 8 | 10 | 68 | 973 |
| Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika madeni mengine | - | (278) | (112) | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | 847 | (424) |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za kifedha** | **8** | **(268)** | **803** | **549** |
| | | | | |
| **Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | | | | |
| **Ongezeko /punguzo katika fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | **(1,669)** | **(154)** | **(425)** | **3,262** |
| Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/mwaka | 11,893 | 12,047 | 10,649 | 7,387 |
| **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **10,224** | **11,893** | **10,224** | **10,649** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI, 2023

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya kwanza inayoanza 01.01.2023** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,937** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato 30.06.2023 | 0 | 0 | 765 | 0 | 0 | 0 | **765** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 18 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **18** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | **0** | **0** | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | **0** | **0** | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | **(211)** | 0 | **0** | 0 | **(211)** |
| **Salio la mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka 30.06.2023** | **10,227** | **17** | **1,571** | **596** | **30** | **68** | **12,509** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2022** | **10,094** | **17** | **(766)** | **1234** | **30** | **100** | **10,709** |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | **1,145** | 0 | 0 | 0 | **1,145** |
| Miamala na wanahisa | 115 | **0** | 0 | 0 | 0 | 0 | **115** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya juu ya hisa | 0 | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | **638** | **(638)** | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | -32 | **(32)** |
| Kodi ya mwaka uliopita | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2022** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,937** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO YA MWAKA ULIOISHIA 30.06.2023

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Mr. Samwel A. Wado **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | S. Wado | 25th Julai, 2023 |
| Mrs. Anitha J. Mnkeni **(Idara Ya Fedha)** | A. Mnkeni | 25th Julai, 2023 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. Mr. Wilson Ndesanjo **(Mwenyekiti wa Bodi)** | W .Ndesanjo | 25th Julai, 2023 |
| 2. Mr. Munguatosha M. Makyao **(Mkurugenzi)** | M.Makyao | 25th Julai, 2023 |

**UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:**

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services,all over the Country-Umoja Switch*

CARING FOR FAMILY ECONOMY

217513602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Takwimu za uhalifu kwa watoto zinashtua

**TAKWIMU** zilizotolewa na Mahakama ya Watoto kuhusu makosa wanayofanya wanaopelekwa kwenye mahakama hiyo zinashtua na ni muhimu kwa wazazi kufanya kazi ya ziada ili kukomesha.

Makosa yaliyotajwa kufanywa na watoto hao ni ulawiti, unyang'anyi wa kutumia silaha, mauaji, wizi na matusi ambayo hufanywa zaidi na watoto hasa wa kiume.

Kinachosikitisha zaidi ni asilimia kubwa ya watoto wa kiume wanaofikishwa katika Mahakama ya Watoto jijini Dar es Salaam, wanashtakiwa kwa makosa ya ulawiti.

Mahakama hiyo inafafanua kuwa aina hiyo ya uhalifu kwa watoto inachangiwa na malezi duni, makundi rika pamoja na umaskini kwa kipato cha familia.

Kwa sababu zilizotajwa kuchangia makosa hayo kufanywa na watoto ni dhahiri kuwa wazazi wanapaswa kuchukua hatua kuwafuatilia watoto wao kwa karibu zaidi ili wasiendelee kupotea.

Kwa mujibu wa mahakama hiyo, watoto wanaotuhumiwa kwa makosa hayo wamethibitika kuyatenda kweli.

Takwimu zilizotolewa kipindi cha miaka minne iliyopita (2018/2019-2021), jumla ya watoto wa kiume 448 waliopokewa katika mahabusu hiyo, 150 kati yao walikuwa wamefanya unyang'anyi kwa kutumia silaha na 84 walilawiti wenzao.

Makosa mengine yaliyofanywa na watoto wa kiume na idadi yao kwenye mabano ni mauaji (10), wizi (76), matusi (4), kujeruhi (6) na kuingia nchini bila kibali (36).

Watoto wa kike waliofikishwa katika mahabusu hiyo kwa kipindi hicho ni 17 ambao walikuwa wanakabiliwa na makosa ya mauaji (5), kujeruhi (3), bangi (1) na kuingia nchini bila kibali (8).

Pia imebainika vitendo vya ulawiti vinachangiwa na utandawazi, kwa watoto kuona kwenye televisheni au kwenye simu.

Changamoto inayoikabili jamii kwa sasa ni wazazi pamoja na walezi kushindwa kutoa ushirikiano wakati wa mchakato wa marekebisho ya tabia, pale mtoto anapokuwa ametenda kosa.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2022, mahabusu ya mahakama hiyo ilipokea watoto 123, kati yao 48 walikuwa wamefanya uhalifu wa unyang'anyi wa kutumia silaha.

Jiji la Dar es Salaam, maeneo ambayo watoto wanapatikana na makosa hayo ni wanaotoka Bunju, Temeke, Mbagala, Kigamboni, Chanika, Kinyerezi, Bagamoyo, Chalinze, Gongo la Mboto, Kigogo Luhanga, Kibaha, Mburahati, Tandika, Manzese, Mbezi Mwisho na Mbezi Juu.

Na wanaoingia nchini bila kibali wanatoka nchi za Kongo na Burundi, kwa mujibu wa mahakama hiyo.

Kadhalika, katika mahakama nyingine ya watoto Kituo Jumuishi cha Temeke, asilimia kubwa ya kesi wanazopokea hivi sasa ni za ukatili wa kingono na kijinsia. Lakini kwa sasa nyingi ni za kulawiti kwa maana ya mtoto kumwingilia mwingine kinyume cha maumbile. Kwa mujibu wa mahakama hiyo.

Tathmini ya mahakama hiyo imebaini kwamba watoto wanaojihusisha na makosa hayo hutokana na malezi duni ya wazazi au walezi.


Watoto wengi wanashawishiwa na kurubuniwa kwanza kabla ya kufanyiwa vitendo hivyo.

"Yule anayemfanyia tukio (ulawiti), haanzi moja kwa moja bali kuna vishawishi watoto wanafanyiana, kuna wengine wanasema walikuwa wanaangalia picha za ngono na kuambiwa afanye kama alivyoona, wengine wanajifunza kwa wenzao shuleni, kwa hiyo kabla ya tukio lenyewe, kuna vitu vya awali vinafanyika," mmoja wa mahakimu wa mahakama hiyo anasema.

Pia baadhi ya watoto wanajifunza na kufanya uhalifu kutokana na wazazi na walezi wao kutowalea ipasavyo kwa sababu ya majukumu ya kutafuta kipato.

Wazazi na walezi wengi, wanaondoka nyumbani alfajiri wakati ambao watoto nao wanajiandaa kwenda shule na wanarudi wakiwa wamechoka kiasi cha kushindwa kuongea nao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tusipuuze fikra za Ben kwenye elimu

**USIKU** wa kuamikia Julai 24 mwaka 2020, Tanzania ilimpoteza Rais mstaafu Benjamin Mkapa, aliyeongoza awamu ya tatu.

Anaaga dunia akiwa na miaka 81 na sasa inapotimia tena Julai 24, 2023 anatimiza miaka mitatu tangu kufariki.

Katika uhai wake, alitamani mambo kadhaa yafanyike ili kuboresha elimu, mojawapo ikiwa ni kuitishwa kwa mjadala wa kitaifa wa kujadili hali ya elimu kutokana na shule za serikali kuendelea kufanya vibaya katika matokeo ya mitihani ya kitaifa.

Katika ufafanuzi wake, anasema mjadala huo unatakiwa kuhusisha makundi yote ya jamii bila kujali kama ni ya sekta binafsi au ya umma, pamoja na Watanzania wa kawaida, siyo wasomi pekee na aliamini kupitia njia hiyo, suluhu ya kudumu ya vikwazo vya elimu ingepatikana.

Wito wake huo kwa serikali, ulikuwa ni wa mara kadhaa ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita wakati wa uhai wake, akitamani kuona mustakabali wa sekta ya elimu unapatikana, ili watoto waweze kunufaika na elimu.

Sasa ametimiza miaka mitatu tangu afariki, ninadhani Watanzania hawana budi kumuenzi kwa mambo mengi, lakini mojawapo likiwa hilo la kutamani elimu ya Tanzania inaboreshwa zaidi.

Aliamini kuwa kuna janga kwenye elimu kwani alipata taarifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari, mawasilisho ya sekta binafsi, walimu, vyuo binafsi pia alisikia minong'ono kutoka kwa vyuo vya umma kuwa kuna kasoro katika elimu.

Kutokana na mazingira hayo, akatamani kukaitishwe mdahalo wa uwazi ambao ungeshirikisha makundi yote na kusikia maoni yao badala kuwaachia wanataaluma pekee ambao wanaegemea kwenye ujuzi.

Rais huyo mstaafu alisukumwa kutoa ushauri huo kutokana na kile alichosema kuwa baadhi ya Watanzania walimletea taarifa kuwa elimu ni ya chini kuliko nchi za Kenya na Uganda na kwamba alikuwa hafahamu kama kuna ukweli juu ya jambo hilo ndipo akatamani kuwapo mdahalo.

Kwa kuwa bado sekta ya elimu inakabiliwa na vikwazo vingi, hasa katika suala la ukosefu wa ujuzi wa fani mbalimbali unaotakiwa kwa wahitimu wa vyuo, ni vyema kuwapo kwa mjadala wa wazi kujadili hilo.

Ukosefu wa ujuzi kwa wahitimu umekuwa ni kikwazo kinachowakabili na kusababisha washindwe kuingia katika soko la ajira na kuwafanya baadhi yao kuhangaika kutafuta kazi bila mafanikio.

Ninadhani kuna haja ya kumuenzi Mkapa kwa kuitisha mdahalo ambao utavishauri vyuo vikuu kuandaa wanafunzi kwa ujuzi wa fani mbalimbali utakaowawezesha kuingia katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Mojawapo ya mapendekezo yao ni ushirikiano wa karibu kati ya taasisi za elimu ya juu na viwanda au waajiri, ili kuwatengenezea wahitimu ujuzi, ambao unahitajika katika soko la ajira.

Ikumbukwe kuwa nafasi za masomo katika vyuo vya elimu ya juu katika programu za shahada ya kwanza zimeongezeka kutoka 157,770 mwaka 2020/21 hadi 172,168 mwaka 2022/23. Hayo ni kwa mujibu wa Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Profesa Charles Kihampa, kwamba hilo ni ongezeko la nafasi 14,398 sawa na asilimia 9.1.

Katika ufafanuzi wake anasema programu za masomo ambazo zimeruhusiwa kudahili wanafunzi wa shahada ya kwanza zimeongezeka kutoka 686 mwaka 2020/21 hadi 757 mwaka 2022/2023.

Wanaodahiliwa katika shahada ya kwanza wameongezeka kutoka 87,934 mwaka 2020/21 hadi 113,383 mwaka 2022/23 sawa na asilimia 28.9. Idadi ya Wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 259,266 mwaka 2020/21 hadi 295,919 mwaka 2021/22 sawa na asilimia 14.1.

Kwa takwimu hizo, ni wazi idadi ya wahitimju nayo itaongezeka, hivyo suala la wanafunzi kuwa na ujuzi ni la muhimu, ili wanapohitimu wasiende kukaa bali wawe na cha kufanya kupitia ujuzi walionao.

Hivyo kuwapo kwa mdahalo ambao utahusisha wasomi na watu wa kawaida ili kuweka mikakati ya kuinua elimu kama ambavyo Mkapa aliwahi kushauri, ninadhani ni jambo la muhimu.

HABARI KITAIFA

# Tanzania yaonesha mafanikio uimarishaji huduma za jamii

**Na Benny Mwaipaja,**
NEW YORK

TANZANIA imewasilisha Taarifa ya Pili ya Mapitio ya Hiari ya Nchi katika Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, katika Jukwaa la Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa.

Aidha, taarifa hiyo imeonesha mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa malengo hayo ikiwamo kuimarisha huduma za jamii, miundombinu, mapambano dhidi ya umaskini na maradhi pamoja na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Taarifa hiyo imewasilishwa juzi na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, katika Jukwaa hilo la Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, jijini New York nchini Marekani, kwa njia ya video fupi na wasilisho hilo kusimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Sanga.

Alisema kuwa taarifa hiyo ilikuwa inawasilishwa kwa mara ya pili baada ya kufanya hivyo kwa mara ya kwanza mwaka 2019.

Alisema serikali imeendelea kuweka programu na mipango mbalimbali ya kupiga vita umaskini, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya teknolojia, ujenzi wa miji salama, usawa wa kijinsia na mambo mengine, licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali zinazohitaji kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa malengo hayo.

Alitaja baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa kuwa ni pamoja na ongezeko la upatikanaji wa majisafi na salama na takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2021 wastani wa kiwango cha upatikanaji maji maeneo ya vijijini kilipanda hadi kufikia asilimia 74.3 ikilinganishwa na mwaka 2019 kiwango hicho kuwa asilimia 70.1.

Dk. Nchemba alisema kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji na hivi sasa inatekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ya umeme, viwanja vya ndege na barabara. Aidha, huduma za afya, elimu na maji zimeendelea kuboreshwa, huku usalama wa chakula ukiendelea kuimarika pamoja na kuendelea na utekelezaji madhubuti programu mbalimbali za kupambana na umaskini.

Alisema kuwa sekta ya utalii imeendelea kufanya vizuri licha ya changamoto za UVIKO -19 na kwamba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alishiriki katika kutangaza utalii kupitia filamu iitwayo the Tanzania Royal Tour ambapo matokeo ya filamu hiyo yalipelekea idadi ya watalii kutoka nje ya nchi kuongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa ana ongezeko la asilimia 57.7

Dk. Nchemba alisema tangu mwaka 2019 Serikali ilipowasilisha taarifa yake ya kwanza ya Mapitio ya Hiari ya Nchi katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Jukwaa la Juu la Siasa la Umoja wa Mataifa.

Alitoa wito kwa taasisi za fedha na jumuiya ya kimataifa kuweka sera zitakazoongeza ufadhili, misaada na mikopo yenye masharti nafuu itakayosaidia nchi kupata fedha zitakazowezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikijumuisha miundombinu inayotegemea matumizi ya teknolojia, kuimarisha ubunifu na kuongeza tija katika sekta ya kilimo ambayo ni tegemezi kwa makundi mbalimbali yakiwamo ya vijana na kuimarisha haki za wanawake na watoto.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alisema Tanzania itaendelea kuongeza bajeti yake katika kufanikisha malengo ya maendeleo endelevu 2030 na kwamba lengo ni kuhakikisha watu wanapata maendeleo na nchi inakua kiuchumi kwa ajili ya manufaa ya wananchi wote hususan vijana.

# Mwingiliano wanyamapori, binadamu wagharimu maisha watu 1,000 nchini

**Na Salome Kitomari**

JUMLA ya watu 1,069 wamepoteza maisha, 642 kujeruhiwa na wanyamapori kwa kipindi cha mwaka 2012 hadi 2019.

Pia ekari 41,404 ziliharibiwa na mifugo 792 ililiwa huku Sh. 4,670,555,300 zilitumika kulipa fidia kwa wananchi waliokumbwa na madhila ya wanyama.

Hayo yalibainishwa na mwezeshaji wa masuala ya uhifadhi, John Noronha, wakati akiwasilisha mada ya kuishi pamoja kati ya watu na wanyamapori ni kipaumbele cha kitaifa kwa maendeleo endelevu na uhifadhi wa wanyamapori nchini, kwa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari.

Huo ni utekelezaji wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili unaotekelezwa na RTI kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET). Alisema kinachochangia migogoro ni ongezeko la watu na wanyamapori na kwamba ni lazima kuchukua hatua mapema kwa kuwa ifikapo mwaka 2035 Tanzania itakuwa na watu milioni 90 huku ardhi ikiwa ni ile ile.

"Watu wote hawa watahitaji makazi, shughuli za kiuchumi huku maeneo ya uhifadhi yameshatengwa, ni lazima kufikiria nini cha kufanya kuhakikisha tunakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ambao unatekelezwa kwenye kila eneo ili kuepusha migogoro," alisema.

Alisema changamoto kubwa ni wananchi walitangulia kuishi kwenye baadhi ya maeneo ya mapito na mtawanyiko wa wanyama ambayo hayakuwekewa alama na walitambua maeneo yalihifadhiwa, lakini haukuwekwa utaratibu mzuri hadi shughuli za kibinadamu zilivyoongezeka kwa kiasi kikubwa.

"Kumekuwa na upanuzi mkubwa wa mashamba kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2018 sasa wanyama wakipita kwenye shoroba wanakuta mazao wanakula," alisema.

Aidha, alisema awali hifadhi zilikidhi mahitaji ya wanyama, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi au kupungua kwa madini maalum wanalazimika kutoka kwenda kuyafuata maeneo mengine wakipita kwenye njia walizozizoea.

"Tembo ni mnyama mwenye kumbukumbu kubwa sana. Mfano Hifadhi ya Taifa Tarangire eneo lenye chumvi kwa ajili ya wanyama inapatikana Simanjiro, ni lazima watoke kwenda kuifuata wanapotoka wanakutaka na vikwazo kwasababu binadamu ameongeza shughuli za kilimo, ufugaji na makazi," alibainisha.

Kwa mujibu wa Noronha, kuongezeka kwa matumizi ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kumepunguza maji kwenye maeneo yanayokaliwa na wanyama hali inayowalazimu watoke kwenda kuyafuta, na kwamba ni lazima binadamu aweke uwiano kwenye matumizi ya rasilimali kwa faida ya viumbe vyote.

Mtaalamu huyo alisema pia kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye baadhi ya vijiji vinavyopakana na maeneo yaliyohifadhiwa au uliopo kutotekelezwa kumesababisha migogoro baina ya wanyama na binadamu.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wahariri wa habari kuhusu uhifadhi na maliasili kwa ujumla ili wanapopokea habari kutoka kwa waandishi waweze kuziboresha zaidi na kutoa nafasi nzuri katika kuelimisha jamii.

"JET kwa kushirikiana na RTI kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili tunatekeleza mradi huu katika shoroba saba kwa kuelimisha jamii umuhimu wa maeneo hayo, uhifadhi na namna wanashiriki shughuli za kijamii za kuendelea kutunza maliasili," alisema.





## UBALOZI WA UINGEREZA, EUROPEAN UNION, NORWAY NA WATAALAM MBALIMBALI DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Uingereza, European Union, Norway na Wataalam mbalimbali watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha,Magari na Generator tarehe 29 Julai, 2023 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, China base, Hutch, Dresser, Book case, Cabinets, Meza za chakula, Viti, Meza za ofisi, Viti, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Deep Freezer, Washer, Garden table / chair, Computer set, TV Set, Projector, Music systems, Nashuatec MP5002SP & MP6500 Photo copy m/c, A/C split units, Trade Mill, Big Satellite dish complete, Automatic Incubator, Solar system, Water pump etc.

**Magari na genereta yataanza kuuzwa Saa 6:00 mchana**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Rover Discovery 4 S/Wagon | SDV6 Diesel Engine | 2013 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado TX | 1KD Diesel Engine | 2017 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser S/Wagon V8 | GF Petrol Engine | 2001 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon Y61 | TD42 Diesel Engine | 2010 | Umelipwa |
| 1 | VW Amarok TDI Pickup Double Cabin | CNE Diesel Engine | 2012 | Umelipwa |
| 1 | Ford Escosport Station Wagon | FY58 Petrol Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 1 | Mercedes Benz Saloon | E220 Diesel Engine | 2007 | Umelipwa |
| 1 | Komatsu Wheel Loader | W100 Diesel Engine | 1984 | Umelipwa |
| 2 | Generator 40 & 30 KVA – 3Phase | Perkins & John Deere Diesel | 2007 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 26 mpaka 28 Julai 2023, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Genereta atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 4 August, 2023 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

217512302




Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Faithful Joshua (kulia), akitoa maelekezo kuhusu huduma za benki hiyo kwa wakulima walio kwenye vikundi wakati wa mafunzo ya elimu ya fedha na mikopo kwa wanawake wanaojihusisha na kilimo cha mboga mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaahidi kuendelea kuwainua wabunifu nchini

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema itaendelea kuwatambua wabunifu, ikiwa ni pamoja na kubidhaisha teknolojia na ubunifu na kuongeza ufanisi ili kuchagiza maendeleo ya uchumi.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akifunga Maonesho ya 18 ya Vyuo Vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Kwa mwaka huu, maonesho hayo yamebebwa na kaulimbiu: "Kukuza ujuzi nchini kupitia elimu ya juu, Sayansi na Teknolojia kwa uchumi imara na shindani."

Kipanga alisema wizara imetoa mafunzo kwa wabunifu wachanga 83 na kutoa rasilimali fedha kwa wabunifu 23, ili kuendeleza ubunifu na teknolojia kwa lengo la kuziwezesha kufikia hatua ya biashara.

"Kwa sasa tunaishi katika ushindani mkubwa siyo tu wa kiuchumi na kijamii pia, ubunifu wa teknolojia mpya na uvumbuzi wenye lengo la kuboresha na kurahisisha maisha," alisema.

Alisema kuwa taasisi za elimu zina mchango mkubwa kuleta mageuzi ya elimu kwa kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi na maarifa stahiki na shindani katika soko la ajira na kuhimili ushindani wa kikanda na kimataifa.

Hata hivyo, alisema taasisi hizo zinapaswa kujielekeza zaidi katika matumizi ya teknolojia na ubunifu kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22 na 25/26, ambao unasisitiza na kuhimiza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu hususani matumizi ya takwimu, mitambo inayoendesha kompyuta na roboti.

"Ninaamini taasisi za elimu ya juu watatekeleza na kutimiza adhma hii ya serikali. Mpango huo ni nyenzo muhimu ya kuchochea na kukuza maendeleo ya sayansi na teknolojia, hivyo taasisi zijielekeze kwenye utafiti na ubunifu katika maendeleo," alisema.

Alisema kuwa, serikali itaendelea kuwaendeleza na kuwatambua wabunifu sambamba na kubidhaisha ubunifu kwa lengo la kutatua changamoto za kijamii.

Makamu Mwenyekiti wa Tume TCU, Makenya Maboko, alisema wamekuwa wakiandaa maonesho hayo tangu mwaka 2016 kwa lengo la kutoa fursa kwa vyuo vya elimu ya juu kutangaza huduma na kazi wanazofanya katika ustawi wa elimu hiyo.

Alisema wanalenga kujenga na kuimarisha uhusiano baina ya taasisi za elimu ya juu na kutoa fursa kwa wananchi na wadau kuona shughuli zao ikiwamo programu za masomo na kuruhusu kufanya uchaguzi sahihi wapi wanaweza kwenda kujiendeleza.

Alibainisha kuwa, TCU itaendelea kutekeleza majukumu yote ya serikali kama yalivyoainishwa katika sera, mipango na mikakati ya maendeleo ya nchi katika masuala yote yanayohusu maendeleo ya elimu ya juu.

Alisema kuwa Tume itahakikisha wanaimarisha mifumo ya udhibiti ubora ya ndani ya vyuo vikuu ili waweze kutoa elimu inayokidhi mahitaji, viwango vya ubora kimataifa, kikanda na kuzifanya taasisi hizo kuwa chachu ya maendeleo ya taifa.

Kadhalika, alisema kuwa maonyesho hayo yataendelea kuwa chachu ya kuongeza fursa za masomo ya elimu ya juu kwa wahitimu wa ndani na nje ya nchi kuchagiza ushindani baina ya taasisi na kuinua viwango vya ubora.

# Segerea yapewa bil. 28/- kuendeleza jimbo

**Na Pilly Kigome**

JIMBO la Segerea limeingiziwa Sh. bilioni 28 za kuendeleza jimbo hilo katika mwaka wa fedha 2021- 2023.

Tayari shule nne za sekondari ujenzi umeshakamilika katika kata ya Kiwalani, Buguruni, Bonyokwa na Kipawa.

Shule zingine nne za sekondari ujenzi unaendelea mbili katika kata ya Liwiti, Bonyokwa na Kipawa ambazo zitakuwa katika mfumo wa ghorofa.

Shule za msingi wapo katika ujenzi wa shule zingine mbili mpya katika kata ya Mnyamani na Kisuru Mpya.

Mbunge wa jimbo hilo, Bonnah Kamoli, alitoa taarifa hio katika mkutano wa hadhara uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, Kata ya Kinyerezi stendi.

Kamoli alisema, fedha hizo wameelekeza katika miundombinu ya elimu na tayari wameshaanza mradi mkubwa wa Mradi wa Maendeleo Jiji la Dar es Salaam (DMDP) ambao asilimia 30 umeshakamilika na 70 utaanza baadaye.

Alisema tayari wameshaanza kujenga vituo vya afya katika Kata ya Segerea, Mnyamani na Kinyerezi.

Pia mradi wa ujenzi wa barabara kiwango cha lami itokayo Bonyokwa Segerea kilomita 3.2 tayari Rais Samia ameshaupitisha.

Alisema wanaishukuru serikali kwa kuwapatia fedha hizo katika jimbo hilo kwa kuwa awali 2015 - 2020 hali ya miundombinu katika jimbo hilo haikuwa nzuri.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Abbasi Mtemvu, alisema watakamilisha miradi yote korofi ikiwamo ya maji katika kata za jimbo hilo.

Mtemvu aliwataka wananchi wa jimbo hilo kuwa na imani kubwa na mbunge kwa kuwa ni mtu wa mfano kupigania jimbo lake kutokana na miradi mingi kuwa katika ngazi za kutekelezwa na mingine ikiwa imeshakamilika.

# Wananchi waomba kujengewa zahanati, shule

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI wa Kitongoji cha Chiuwe, Kijiji cha Mnamba, Kata ya Namupa, Wilaya na Mkoa wa Lindi, wanaiomba serikali kuwajengea zahanati na shule ili kuwaondolea tatizo la kufuata huduma hizo umbali mrefu.

Pia wameomba kitongoji chao kipatiwe namba ya utambulisho kiweze kufahamika kisheria kama ilivyo maeneo mengine nchini.

Maombi hayo yamewasilishwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, wakati wa mkutano wa hadhara kutambulisha mradi wa maji vijiji 56 wilaya za Lindi, Nachingwea na Ruangwa unaotekelezwa na kampuni ya STC Construction Co. Ltd na Emirate Building Co. Ltd kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 119.1.

Wakiwasilisha maombi yao kwa njia ya mabango, wakazi hao wameishukuru serikali kupeleka mradi wa ujenzi wa chujio la kusafisha ubora wa maji katika eneo lao, huku wakiomba kupatiwa zahanati, shule na namba ili kitambuliwe kisheria kama ilivyo maeneo mengine.

Aidha, wameeleza kwamba wanapopatwa na tatizo la homa hulazimika kutembea mwendo mrefu kufuata huduma za matibabu katika Hospitali ya Mission Nyangao iliyopo zaidi ya kilomita 30 na maeneo wanayoishi.

Wakazi hao pia wanaomba kupatiwa shule kwa ajili ya kuwapunguzia watoto wao kutembea mwendo mrefu kufuata elimu Kijiji cha Mnamba kufuata elimu, jambo walilodai ni hatari kwa usalama wa maisha ya vijana wao kutokana na misitu mikubwa iliyojaa wanyama wakali.

"Tunaipongeza serikali kuleta mradi ndani ya kitongoji hiki, tunaomba tuletewe zahanati, shule namba ili kitongoji chetu kitambulike kisheria," moja ya mabango hayo yalieleza.

Ndemanga aliwahakikishia wananchi hao kwamba serikali ipo tayari kutekeleza mahitaji ya wananchi hao kwa kuwa inatambua ili taifa liwe na maendeleo ni lazima raia wake wawe na elimu na afya bora na kuwataka kuandaa maeneo yatakayotumika kujenga zahanati na shule.

Aliwataka pia wawe tayari kujitokeza nguvu kazi zao katika kushiriki ukusanyaji wa mawe, mchanga, kuteka maji na kuchimba mitaro wakati wa ujenzi.

"Mnaomba kitu bora kwani dunia ya sasa bila elimu na afya njema ni tatizo, lakini nyinyi mmeliona hilo muwe tayari kushiriki nguvu kazi zenu wakati wa utekelezaji wake," alisema Ndemanga.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Mazingira (RUWASA), Wilaya ya Lindi, Iddi Pazi, alisema utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kituo cha kusafisha ubora wa maji kinachojengwa ndani ya Kitongoji cha Chiuwe, Kijiji cha Mnumba, Kata ya Namupa.

Alisema mradi huo utakapokamilika utasaidia kuondoa tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wakazi wa vijiji 56 vikiwamo 34 katika Wilaya ya Ruangwa 21, Nachingwea na kimoja Lindi.



## Serikali yapata mwarobaini waraibu dawa za kulevya

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SERIKALI imeweka mpango mkakati wa kujenga kituo kikubwa cha huduma za utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya jijini Dodoma ili waweze kupata mafunzo ya ujasiriamali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Hayo yalisemwa juzi na Kamishna Msaidizi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kitengo cha Tiba na Huduma za Utengamao, Dk. Cassian Nyandindi, kwenye hafla ya waraibu waliopata nafuu mkoani Tanga ili waweze kuwapeleka wenzao kujiunga na huduma za tiba na utengemao.

Alisema mamlaka hiyo ni taasisi ya Serikali iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohughulia na kuratibu masuala yanayohusiana na tatizo la dawa za kulevya hapa nchini

Vilevile alisema hatua hiyo, ni moja ya jitihada za dhati zinazofanywa na Serikali kupanua na kuimarisha huduma za tiba kwa wagonjwa hao huku akieleza kuwa sasa kuna jumla ya vituo 15 vinavyohudumia zaidi ya watu 14,500.

"Mikakati yetu ni kupanua huduma hizo, ili kuweza kuwafikia waraibu wengi zaidi katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kwa lengo la kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Aidha alisema Serikali inawasaidia waraibu hao kupata mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo mbalimbali ili wajikimu na kukuza pato la taifa kwa kuwa huo ni mikakati walioweka katika mpango wa kupanua huduma hizo za utengamao. Akizungumzia kuhusu vituo cha waraibu hapa nchini, alisema vinasaidia kuondokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa kutoa matibabu mbalimbali ikiwamo ya ukimwi, kifua kikuu, homa ya ini pamoja na matatizo ya akili.

Pia wanapokwenda kwenye vituo hivyo wanapata fursa ya kupata wanasii wanaowabadilisha tabia na kuachana na tabia za waraibu kupunguza uhalifu, kuimarisha uhusiano kwenye ngazi ya jamii na kupata mafunzo ya ujasiriamali.

Katibu Mtendaji wa Asasi ya Kiraia ya Gift Of Hope, Saidi Bandawe, alisema walikuwa na kikao kazi na wadau mbalimbali na jamii wanayokwenda kuiwezesha kwa ajili ya kufanya huduma kwa ajili ya watumiaji wa dawa hizo.

Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga, Abdurhaman Shillow, akizungumza wakati akifungua hafla hiyo, alisema Tanga haifurahii kuona inashika nafasi ya pili kwa matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Alisema wao kama viongozi suala la madawa ya kulevya Tanga, halina nafasi huku akimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuangalia tatizo lililopo kwenye Jiji hilo. "Tuna amini itakuwa mwarobaini na kulitatua tatizo hili,kwa kiwango kikubwa Wilaya ya Tanga, kwa kuwa anaijua mitandao yake anajua mahali sahihi na anajua namna ya kupambana nalo. "Lakini hakuna kiongozi anayependa kuongoza watu nguvu na kazi inapotea kwa kuzama kwenye uraibu na dawa za kulevya hivyo tunaamini historia ya Tanga kuwa wa pili kutumika kama njia ya kuingia na kupitisha dawa za kulevya haitakuwapo tena," alisema.

# Serikali yajizatiti kutokomeza unyanyasaji vyuo vikuu

**Na Allan Isack,** MONDULI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema serikali itaendelea kuzingatia suala la usalama na ulinzi kwa watoto kwenye taasisi za elimu na vyuo nchini, ili kuhakikisha kwamba hakuna unyanyasaji wa kijinsia utakaotendeka.

Prof. Mkenda aliyasema hayo juzi mkoani Arusha wakati akizindua mwongozo wa ulinzi na usalama kwa wanawake na vijana katika vyuo vya maendeleo ya wananchi, vyuo vya ualimu na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC), Mto wa Mbu wilayani Monduli mkoani humo.

Alisema suala la usalama kwa wanafunzi ni jambo muhimu hivyo aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto vyuoni na kuwa na imani na usalama wao.

Aidha, alisema mwongozo huo umezingatia mahitaji na utakwenda kuongeza umakini katika suala zima la kuwalinda wanafunzi katika jamii.

Katika hatua nyingine alishukuru Serikali ya Canada kwa ufadhili wa dola za Marekani milioni 25 ambazo zitakazotumika kutoa elimu kwa wasichana ili waweze kushiriki kikamilifu katika mafunzo na shughuli za kiuchumi.

Rais na Mkurugenzi Mkuu wa Jumuiya na Taasisi za Vyuo vya Canada (ciCan), Denise Amyot, alisema katika mradi wa ESP, wanazingatia sana suala la uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake na wasichana kwenda sambamba na lengo namba tano la maendeleo endelevu linalohusu usawa wa kijinsia.

"Tunajivunia kupata mafanikio haya ambayo yatakuwa na mchango mkubwa katika maisha ya vijana wa kike na kiume," alisema. Pia alisema vyuo 12 viko katika mpango wa kutoa elimu ya ufundi stadi kwa wataalamu kutoka Canada kwa ajili ya kuhakikisha vyuo hivyo vinafikia malengo yake.

Aidha, alisema mradi huo wa miaka saba (2021-2028), unafadhiliwa na Serikali ya Canada na utatekelezwa na Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Canada (CIC), kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Tanzania (MOEST),kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (DTVET).

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Dollar Rajamu, alisema serikali imelenga kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu nchini kwa kuleta matokeo chanya.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (katikati), akimkabidhi cheti cha pongezi Mkuu wa Shule ya Sekondari Naisinyai wilayani Simanjiro, William Ombay, baada ya shule hiyo kufaulisha wanafunzi wote 33 wa kidato cha sita, mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yaagiza usimamizi uendeshaji huduma za afya

**Na Allan Isack, ARUSHA**

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia Afya, Dk. Wilson Mahera, ameagiza timu za uendeshaji wa huduma za afya nchini kusimamia mfumo mzima wa upatikanaji wa dawa na kuondoa mianya ya upotevu wake.

Vilevile ameziagiza kuimarisha dhana nzima ya ununuzi wa bidhaa za afya kwa kutumia takwimu zilizo sahihi.

Dk.Mahera, alitoa agizo hilo, jana jijini Arusha wakati akifungua mafunzo ya Menejimenti, Uongozi na Utawala ya kuwajengea uwezo wataalamu wa afya 43 kutoka halmashauri 11 za Mkoa wa Tanga.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo timu za uendeshaji wa huduma za afya katika halmashauri (CHMT) na vituo vya kutolea huduma (HMT), kwenye uongozi, utawala na usimamizi wa rasilimali na ubora wa huduma ili kuleta tija na ufanisi katika uendeshaji wa vituo hivyo, ustawi wa jamii na lishe.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuzingatia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo kwa sasa inafanyiwa mapitio na Mpango Mkakati wa tano wa Sekta ya Afya (2021-2026) ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kwa kiwango na ubora unaostahili.

"Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa kufanya ukarabati, ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaa tiba pamoja na samani, ujenzi wa nyumba za watumishi na kuajiri watumishi wapya," alisema Dk. Mahera.

Aidha, aliwataka wataalamu hao kuwa na usimamizi thabiti katika uwekezaji unaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, katika sekta ya afya na ustawi wa jamii.

Alisema endapo kutabainika kuwapo kwa uzembe katika maeneo ya usimamizi kulingana na uwekezaji serikali itachukua hatua kali kwa wahusika wote.

Dk. Mahela alisema katika kuimarisha utoaji huduma hizo, kupitia dhana ya ugatuaji wa madaraka tangu mwaka wa fedha 2007 serikali iliamua kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kwa wakati.

Alisema upatikanaji wa huduma bora utaongeza ushiriki wa wananchi kufanya maamuzi na ari ya utendaji kwa watumishi.


"Tuendelee kusimamia ipasavyo mfumo huu, kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi kwa kuwa itasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji na uwajibikaji katika sekta ya afya.

Aidha Dk. Mahera, alisema Ofisi ya Rais TAMISEMI, imeandaa na tunawaendelea kutekeleza mpango kazi wa uboreshaji wa huduma wenye maeneo 11 ya kimkakati.

Alisema hadi sasa kuna vituo vya kutolea huduma za afyangazi ya msingi zaidi ya 7000, vituo vya afya zaidi ya 700, hospitali za wilaya 188 na zahanati 5000.

Naye Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha, Mounti Meru, Alex Ernest, alisema serikali imewekeza katika ujenzi wa miundombinu na kununua vifaa tiba vya kisasa katika hospitali hiyo ili kuhakikisha wanatoa huduma bora.

Alisema hospitali hiyo ilipatiwa Sh. bilioni 5.4 zilizotumika kuboresha miundombinu ya majengo na kununua vifaa tiba.



# Bil.2.7/- kumaliza tatizo upatikanaji wa maji Msalala

**Na Mwandishi Wetu,**
MSALALA

MRADI wa maji Bugarama uliopo Wilaya ya Msalala Mkoa wa Shinyanga wenye thamani ya Shilingi bilioni 2.7 upo mbioni kukamilika na kuwa mkombozi kwa maelfu ya wananchi wa maeneo hayo.

Juzi Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alitembelea mradi huo na kukagua ufanisi wa utekelezaji wake na kuonyesha kuridhishwa na kazi iliyofanywa na mkandarasi katika mradi huo.

"Nitoe pongezi kwa kazi nzuri inayoendelea hapa. Mkandarasi anafanya vizuri na ameahidi ifikapo Septemba 21, mwaka huu kazi itakuwa imekamilika na kutukabidhi mradi wetu kwa ajili ya kuondoa adha ya upatikanaji wa maji Bugarama," alisema Mhandisi Luhemeja.

Luhemeja aliwataka Wakala ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, kuhakikisha usimamizi mzuri wa fedha zitokanazo na miradi hii kwa kuingia katika mifumo rasmi ya usimamizi ya serikali na kuondoa dalili zote za upotevu wa fedha.

"RUWASA sasa wanatakiwa kubadilisha fikra katika utoaji wa huduma, badala ya kuwaza kuweka vituo vya kuchotea maji na kuunda vikundi vya jamii ya watumia maji wanapaswa kufikisha maji majumbani kwa wateja," alisema Luhemeja.

Mratibu wa mradi huo, Mhandisi Mashaka Sita, alisema kutokana na ongezeko la watu katika eneo la Bugarama na vijiji vya pembeni waliamua kutekeleza mradi huo ili kukidhi mahitaji ya utatikanaji wa huduma hiyo.

## Luhemeja aagiza mkandarasi kuvunjiwa mkataba, kurudisha fedha

**Na Marco Maduhu,**
KAHAMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Cyprian Luhemeja, ameagiza mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji katika Kijiji cha Mwaningi Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama kuvunjiwa mkataba, kurudisha fedha alizolipwa.

Mkandarasi huo ni kutoka Kampuni ya Pet Cooperation ambaye anadaiwa kulipwa pesa za mradi huo lakini hadi sasa hajakamilisha kazi, hayupo eneo la mradi. Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki akiwa ziarani kukagua utekelezaji wa miradi ya maji kwa wananchi wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga. Alisema serikali haitavumilia kuendelea kufanya kazi na makandarasi ambao wamekuwa wakitekeleza miradi, huku wananchi wakiendelea kutumia maji machafu na kuagiza mkandarasi huyo kutokupewa kazi yoyote ya ujenzi wa miradi ya maji nchini.

"Kwanza naagiza mkandarasi huyu aripoti kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama siku ya Jumatatu (jana) vilevile arudishe fedha za serikali ambazo tayari alikuwa ameshachukua," alisema Mhandisi Luhemeja.

Aidha, alimwagiza Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Julieth Payovela, kuchukua fedha itakayorudishwa na mkandarasi huyo kuwapatia wananchi ili wachimbe mitaro ya kupitisha mabomba ya maji ya mradi huo, pia ahakikishe unakamilika ifikapo Oktoba.

Aidha, Meneja wa RUWASA mkoani humo Mhandisi Julieth Payovela, alisema, mradi huo ulianza kutekelezwa Februari 2022 na ulitarajiwa kukamilika Juni 2023 ukigharimu Sh.bilioni 2.2, lakini mkandarasi huyo ameutelekeza huku akiwa ameshachukua baadhi ya fedha, akitafutwa hapatikani.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Mwaningi akiwamo Malita Charles, wakizungumza na Nipashe walisema wanakabiliwa na uhaba wa majisafi na salama na wamekuwa wakitumia maji ya mabwawa kwa matumizi yote ya nyumbani ikiwamo kunywa.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wapili kulia) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mafuta ya Puma Tanzania Fatma Abdallah (kushoto) baada ya Waziri kutembela eneo la kuhifadhia mafuta ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Puma Energy yawatoa hofu Watanzania

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya kuripotiwa kuwepo kwa uhaba wa mafuta ya petroli katika baadhi ya mikoa nchini, kampuni ya Puma Energy imesema ina akiba ya kutosha kusambaza mafuta sehemu mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Fatma Abdallah, amesema mwezi huu kumekuwa na mahitaji makubwa ya mafuta, kwamba hadi jana wameuza petroli na dizeli zaidi ya lita milioni 36.

Amesema hali hiyo ni tofauti na mwaka jana ambapo mpaka kufikia kipindi kama hiki walikuwa wameuza mafuta lita milioni 30.

"Kama ambavyo serikali imesema mafuta yapo, sisi kama Puma Energy tunawahakikishia Watanzania mafuta yapo ya kutosha," alisema Fatma.

Alisema mpaka kufika mwisho wa mwezi huu wanatarajia kuuza zaidi ya lita milioni 50 za mafuta katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Aidha, alisema kuna meli zipo njiani zinakuja nchini ambapo zina mzigo wa kampuni hiyo kiasi cha lita milioni 16 ambazo wanatarajia kupakua siku chache zijazo.

" Agosti tutapata mafuta ya dizeli na petroli lita zaidi ya milioni 60, niwatoe hofu wauzaji wakubwa na wadogo mafuta yapo ya kutosha na tunashirikiana kwa ukaribu na Serikali," alisema Fatma.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema changamoto waliyonayo mpaka sasa ni uhaba wa dola za Marekani akiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia ili upatikanaji wake uwe mwepesi.

# Serikali kuendeleza ushirikiano na AZAKI

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendeleza ushirikiano na Asasi za Kiraia (AZAKI) pamoja na wadau wa maendeleo katika kufanikisha shughuli za kimaendeleo, hususani katika maeneo yasiyofikika.

Hayo yamebainishwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christine Mndeme, wakati wa uzinduzi wa kanzidata za machinga uliofanyika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha makundi yote yanafikika na kuhudumiwa kwa urahisi.

Alieleza kuwa mkakati wa serikali ni kuhakikisha kuwa, inaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ili kuhakikisha uchumi wa nchi unakua na kukuza kipato cha kila Mtanzania.

Alieleza kuwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan serikali imefanikiwa kuyafikia makundi mbalimbali wakiwamo machinga.

Kadhalika, alisema kuwa serikali kwa kushirikiana na kampuni ya bima ya TIVA walifanya utafiti na kubaini kuwa, makundi mengi hayapati huduma za afya wakiwamo machinga kutokana na kutokuwa katika mfumo wa kanzi data.

Aliongeza kutokana na hali hiyo waliweza kuwaongoza kwenye kanzi data ambayo ina taarifa za machinga wote kuanzia vijijini hadi mijini, jambo ambalo litakuwa rahisi kwa serikali kupeleka huduma za Maendeleo.

Mkurugenzi wa Huduma za Fedha na Masoko wa Kampuni ya TIVA, Mark Irunde, alisema: "Tulifanya utafiti tukagundua kuwa idadi kubwa ya wananchi hawamo kwenye mfumo wa bima ya afya kutokana na kukosekana kwa taarifa zao, wakiwamo machinga."

Kutokana na hali hiyo alisema kuwa waliamua kuandaa kanzi data kwa kushirikiana na kampuni za mitandao ya mawasiliano ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za kila mwananchi kwa maeneo ya mijini na vijinini.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Umoja wa Machinga nchini (SHIUMA), Ernest Masaju alisema kuwa machinga ni sehemu ya kundi ambalo lilisahaulika katika mfumo wa kanzi data jambo ambalo lilikuwa gumu kujua mahali walipo na idadi yao.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 25, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

## Hii ndiyo siri kisiwa cha maisha marefu


Ukurasa 12

NZUNDA NA BUBERWA
Wagunduzi wanaodhihirisha jinsi plastiki ilivyo mali


Ukurasa 13

Miradi ya kiuchumi ilivyofanikisha kufukuza tembo, kunufaisha jamii

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE, ALIYEKUWA MARA

# Ni kicheko wanaokwenda fomu 'V' mwezi ujao...

•Watakapoanza ndani ya madarasa mapya 1,090 yaliyojengwa mikoa yote

KATIKA juhudi za kuandaa miundombinu ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha tano mwezi ujao, kampuni ya Twiga Mineral Cooperation, inawajenga vyumba vya madarasa zaidi ya 1,000 kwa nchi nzima.

Ujenzi huo, unaofanywa na kampuni ya kuchimba madini katika mgodi wa North Mara ya Barrick kwa kushirikiana na serikali, wawili hao wanamiliki kwa ubia kampuni ya Twiga Mineral Cooperation.

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Dk. Mark Bristow, anasema kwa pamoja watajenga madarasa 1,090 yatakayotumiwa na wanafunzi 49,000, kazi itakayofanywa katika shule 161.

Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) mapema Machi mwaka huu lilitangaza matokeo ya kidato cha nne na baadhi ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha tano wataanza masomo mwezi ujao.




Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow (katikati), akizungumzia faida za uzalishaji katika migodi ya Bulyanhuru na North Mara kwa ubia na serikali kupitia kampuni ya Twiga Mineral Corporation. Kulia ni Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa na Meneja wa Barrick Tanzania, Melkiory Ngido. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, anaongeza kuwa kwa ushirikiano na kwa pamoja kampuni hizo zimetoa dola za Marekani milioni 30 (zaidi ya Shilingi bilioni 73) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo mkubwa.

Anaongeza kuwa ujenzi wa vyumba vya madarasa unalenga kufanikisha programu maalum ya kusongesha mbele mustakabali wa shule (future forward school programme).

"Programu hii ni maalumu kufanikisha shule kuchukua wanafunzi 49,000 wanaotarajiwa kuanza kidato cha tano mwaka huu. Tunaamini kuwa kujengwa vyumba hivi tutakuwa tumechangia juhudi za serikali katika kuinua elimu nchi nzima," anasema Dk. Bristow.

Halikadhalika, anaongeza kuwa kampuni hizo zimeweka mbele suala la elimu na ndiyo sababu wamekuwa wakisaidiana kuboresha miundombinu ya shule katika vijiji vinavyozunguka migodi yake ya North Mara na Bulyangulu uliopo Kahama mkoani Shinyanga.

"Tutaendelea kuboresha miundombinu ya shule kupitia programu hii lakini pia pale inapohitajika tunafanya hivyo katika vijiji vinavyozunguka migodi kwenye madarasa, nyumba za walimu na hudums nyingine zinazohitajika," anasema Dk. Bristow.

Anasema ushirika wa Barrick na kampuni ya Twiga mbali ya kujenga vyumba hivyo vya madarasa, pia wataendelea kuboresha miundombinu mingine kama barabara na huduma za maji safi na salama katika vijiji vinavyozunguka migodi yake.

"Pamoja na haya yote, lakini kwetu kipaumbele cha kwanza ni elimu, tunaamini katika kwenye kuelimika ndipo vijana wanapoanza kutengeneza ndoto zao na kuzifikia," anasema Rais na Mtendaji Mkuu.

Anaungwa mkono na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, anayesema mkoa huo utaendelea kushirikiana na wawekezaji wakiwamo Barrick na kufanikisha miradi mbalimbali ya wananchi watakayoianzisha.

"Tunaunga mkono moja kwa moja mradi huu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa, hii ni kwa sababu inaenda kuongeza nguvu kwa jitihada za Rais Samia Samia Suluhu Hassan kuboresha elimu ya watoto wa Tanzania," anasema Mtanda.

"Kazi yetu ni kusimamia maendeleo ndani ya mkoa, tutafanya hivyo na kuimarisha mahusiano mema kati ya wawekezaji na wananchi, lakini pia tunaunga mkono miradi yote ambayo ina faida kwa wananchi na serikali," anasema Mtanda.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu katika elimu anaeleza kuwa imevisaidia vijiji vinavyozunguka mgodi wa North Mara kwa kujengewa madarasa na miundombinu mingine.

"Tukipewa miradi kama hii ambayo inagusa moja kwa moja jamii yetu, mfano ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu na vifaa mashuleni ni miradi ambayo inakwenda kunufaisha jamii moja kwa moja, lakini inaisaidia na kufanikisha juhudi za serikali za kuwafikia wananchi na kuwapa huduma muhimu," anasema Mtanga.

Anasema kwa Wilaya ya Tarime Vijijni unapopatikana mgodi wa North Mara vijiji vya Nyangoto, Nyabichune, Mjini Kati pamoja na Matongo vimenufaika na miradi hiyo ya Barrick.

Anasema zipo shule zilizojengwa katika vijiji hivyo na kuboresha miundo mbinu yake na kushukuru uwekezaji huo ambao unasaidia Watanzania kwa sasa na vizazi vijavyo.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA
NA CHRISTINA MWAKANGALE

NZUNDA NA BUBERWA

# Wagunduzi wanaodhihirisha jinsi plastiki ilivyo mali

WAKATI wowote Tanzania inaweza kuanza kujivunia matunda ya ubunifu na ugunduzi unaoendelezwa na kukuzwa na viatamizi (incubators) katika vyuo vikuu kikiwamo cha Dar- Es-Salaam.

Ndivyo unavyoweza kusema ukifuatilia baadhi ya kazi za wagunduzi wanaosimamiwa na UDSM na kulelewa na kiatamizi chuoni hapo kama wanavyoeleza wagunduzi wake wanafunzi wa uhandisi, Daud Nzunda na Laetus Buberwa.

Wawili hawa wamebuni namna ya kuzalisha umeme kwa kutumia uji au kimiminika kinachopatikana baada ya kuyeyusha chupa za plastiki zilizotumika na kutupwa mitaani.

Wakizungumza na Nipashe kwenye maonesho ya Sabasaba, jijini Dar es Salaam wanasema wanazitumia taka hizo ambazo haziyeyuki ardhini wala kuoza kwa urahisi, kuzalisha nishati hiyo, kwa matumizi tofauti, kama kuchaji vifaa vya kielektroniki.

Nzunda, anayesomea uhandisi wa bayoteknolojia ambayo ni taaluma zinazohusisha sayansi na uhandisi kwa kutumia viumbe hai, seli, tishu na sehemu zao mbalimbali kupata bidhaa na huduma bora na zenye ufanisi zaidi ili kurahisi maisha ya binadamu.

Anasema: "Sisi wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hapa Sabasaba tumekuja na ubunifu wa mashine inayotengeneza umeme wa matumizi ya nyumbani, lakini gesi ya kupikia ikitumia chupa za plastiki."

Anaongeza: "Kwa hiyo badala ya kuweka petroli au dizeli au gesi, tunatumia chupa za plastiki mashine inayozichakata kuzalisha umeme unaotumika nyumbani."

**MWANZO WA UBUNIFU**

Nzunda anasema wazo la kuunda mashine hiyo linakuja baada ya kubaini tatizo la kupatikana nishati umeme, hasa kwa ambao hawajafikiwa na huduma hiyo. Lakini ni katika kutafuta mbinu ya kutunza mazingira, kwa kuwa chupa za plastiki hutupwa ovyo na kuharibu mfumo wa ekolojia angani, juu na chini ya ardhi pamoja na ndani ya maji.



Mainjinia Daud Nzunda na Laetus Buberwa, wakizungumzia mashine yao kwenye maonyesho ya Sabasaba. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Matumizi makubwa ya plastiki yameleta madhara mengi kwa mazingira, kwanza inachukua muda mrefu kuoza, inachafua mazingira kwa njia nyingi za uzalishaji wa gesi chafu, zichafua maji, kuharibu maisha ardhini, athari kwa viumbe hai na hewa inapo kutoa kemikali hatari na sumu ambazo zina madhara kwa afya ya binadamu na viumbe hai pale zinapochomwa.

"Tumetafakari hiyo baada ya kuona kwenye jamii yetu kumekuwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira kutokana na taka za plastiki kusambaa mitaani lakini pamoja na hizo changamoto za umeme. Tumebuni mashine hii ambayo inatengeneza umeme kwa kutumia vitu hivyo ambavyo vinapatikana karibu kila mahali," anaongeza.

Mashine hiyo, inafanya kazi pale unapochukua chupa za plastiki ukaziwasha moto zinapoyeyuka na kuwa kimiminika, mashine inakichakata kuzuia kisigande.



Taka za plastiki zikitapakaa kwenye fukwe. **PICHA: MTANDAO**

Anaongeza kuwa kisha kinaingizwa kwenye mota ndani ya injini, badala ya kutumia petroli au dizeli kinakuwa ndiyo nguvu ya mashine hiyo.

Anafafanua zaidi kwamba, kama injini zinazotumia dizeli au petroli ndivyo mashine hiyo inavyofanya kazi ikitumia uji wa plastiki, kwa ajili ya kutengeneza umeme na pia ni kizito kidogo ikilinganishwa na petroli au dizeli.

Nzunda anaeleza uwezo wa mashine hiyo akisema, kwenye injini wameifanyia maboresho ili iendane na mtambo huo. Aidha, ina uwezo wa kutoa umeme wa kilowati 1.5 au wati 1,500 ambayo inaweza kitumika kuwasha taa, feni, televisheni, redio na televisheni.

Mhandisi huyo anabainisha kuwa kama anatokea mwenye kuhitaji mfumo wa umeme mkubwa, mteja huyo wanamtengenezea mashine kulingana na mahitaji yake.

Anasema uwezo wa mashine hiyo ni kutoa volti 24 lakini pia unaweza kuitumia kuendesha vifaa vinavyotumia umeme jua au sola.

Kadhalika, anasema mashine hiyo inatumia kilo moja ya plastiki na ina uwezo wa kutengeneza umeme ambao utatumika kwa takribani saa sita, uwezo wake ni kubeba kilo15 na kuwa chanzo cha umeme wa saa 90 takribani siku nne.

"Kwa hiyo ukiwa na kilo 15 hapo inakuwa na muda mrefu sana. Hii mashine hata kama matumizi ni makubwa utapata nishati ya uhakika. Tumetengeneza itumike pale ambao umeme wa TANESCO a unakatikatika, ukikatika unaitumia mashine au LUKU imemalizika mahine hii inakufaa, au kama kuna mvua umeme wa sola unakwama kwa vile jua halipatikani la kutosha. Mashine hii itakufaa pia," anaeleza Nzunda.

**MAJARIBIO**

Msomi huyo anasema kwa kuwa mashine hiyo ni ubunifu mpya, lazima kuifanyia zaidi majaribio na kamba wameanzia majaribio chuoni hapo na baadhi yanafanyika nje ya UDSM ili kubaini utendaji kazi wake kiuhalisia na kiufanisi.

"Kwa sasa hivi tumeanza majaribio na tunaifanyia kazi maeneo mbalimbali kama vile kwenye migahawa ya chakula chuoni hapa cafeteria, jirani Changanyikeni pia mitaani tunazijaribu River Side Ubungo," anasema Nzunda.

# NI KICHEKO WANAOKWENDA FOMU 'V' MWEZI UJAO...

**INATOKA UK.11**

Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, anasema kuwa kuwapo kwa ushirikiano wa kampuni ya Barrick na Twiga Mineral Cooperation kumeleta faida kubwa kwa jamii na serikali pia.

"Baada ya kutekelezwa kwa miradi hii, wananchi sasa tujue na tuwajibike kwa kuwa tunatakiwa kutunza miundombinu inayojengwa kama vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo ambayo wenzetu wa Barrick wanatusaidia kuipata," anasema Naibu Waziri Kiruswa.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, kwa upande wake anawashukuru viongozi wa Barrick na Twiga kwa kutekeleza miradi mbalimbali hususani kwenye seta ya elimu katika wilaya hiyo.

Anasema wananchi wa Tarime Vijijini wanathamini miradi inayotekelezwa na mgodi huo na kuwaomba wananchi kuendelea kuitunza na kuwa na mahusiano mazuri na mgodi huo.

ELIMU

NA SALOME KITOMARI

# Miradi ya kiuchumi ilivyofanikisha kufukuza tembo, kunufaisha jamii

MOJA ya hatari zinazowakabili wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi ni kifo na uharibifu wa mali kuanzia mazao, makazi na kuua mifugo.

Kwa mfano, takwimu za idara ya wanyamapori zinazoanzia mwaka 2012 hadi 2019, zinataja watu waliouawa na wanyama hao ni 1,069.

Aidha, 642 wakajeruhiwa huku ekari 41,404 za mazao mbalimbali zikiharibiwa, mifugo 792 kuuawa na wanyamapori na Shilingi bilioni 4.6 zililipa fidia kwa waathirika.

Uharibifu huo unatokana na wanyama kupita kutoka eneo moja kwenda jingine kutafuta mahitaji, jambo ambalo wadau wanalitafutia ufumbuzi, ikiwamo Taasisi ya Kusimamia Uhifadhi wa Tembo wa Kusini (STEP).

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Shirika la Marekani la USAID kupitia mradi Tuhifadhi Maliasili, wameongoza au kufufua, shoroba ya tembo ya Kilombero inayopewa jina la Nyerere-Selous -Udzungwa.

Kwa zaidi ya miaka 10 ambayo wamefanya kazi kwenye eneo hilo wametumia mbinu mbalimbali kusaidia jamii, ikiwamo kuwa na miradi ya kufukuza tembo ili waendelee na kilimo.

Lakini, STEP imejenga shoroba ya kwanza ya kisasa ambayo itawekewa waya wa umeme na kulazimisha wanyama kupita kwenye njia maalum hifadhi ya taifa Udzungwa kwenda Hifadhi ya Taifa Nyerere hadi Pori la Akiba Selous.

Tayari wananchi wameshalipwa fidia kupisha ujenzi huo katika vijiji vya Kanyenja, Sole na Mang'ula A ambao wana miradi tofauti, pamoja na vikundi vya VIKOBA lengo ni kuwawezesha kiuchumi na kuwa na mbinu za kufukuza tembo.

Mratibu wa mradi wa kuboresha mahusiano kati ya tembo na watu wa STEP, Kim Lim anasema lengo ni kupunguza uharibifu wa mazao unaosababishwa na wanyama na kuwezesha wananchi kujiongezea kipato na kutoa elimu kwa wanafunzi.

"Tunafanyakazi na vikundi saba kwa miradi ya uzio wa mizinga ya nyuki, taa za umeme wa jua na uzio wa mabati kuzuia tembo wasiingie mashambani na vikundi 12 vya VIKOBA kuwezesha wananchi kuona faida ya uhifadhi," anasema.

Kuhusu mizinga Lim anasema wana kikundi wamepewa elimu na kuwezeshwa na sasa wanauza asali na kupata fedha ambazo hugawana kwa kadri ya makubaliano.



Uzio wa mizinga kuwadhibiti tembo umefanikisha kulima maeneo ambayo kwa miaka mingi hayakulimwa kutokana na kupakana na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere. **PICHA: SALOME KITOMARI**

"Kwenye VIKOBA tunafanyakazi na vikundi 12 vyenye wanachama 250 ambao asilimia 50 ni wanawake na vijana, tangu mwaka 2020 hadi sasa vinawasaidia kutatua changamoto zao," anasema.

"Kabla ya VIKOBA hivi kama mwanachama akihitaji mkopo alikuwa anakopa Shilingi 50,000 kwa dhamana ya gunia la mpunga, anayemkopesha anabaki nalo kusubiri bei ipande ambalo analiuza 200,000 hadi 250,000 anapata faida zaidi ya Shilingi 100,000.

Kupitia VIKOBA watu hawachukua mikopo kwa udhamini wa mpunga, wanakopa na kurejesha baada ya miezi mitatu," anafafanua Lim.

Aidha, ndani ya VIKOBA kuna fungu la jamii ambalo mtu akipata dharura kama kufiwa au kuuguliwa anaweza kuchukua mkopo wa dharura.

Kwa mujibu wa Lim, mikopo iliyotolewa kwa VICOBA ni zaidi ya Shilingi 7, 000,000 na wanakikundi walinunua hisa zenye thamani ya Sh. milioni 35, na kwamba kila wakinunua wanatumia kuchukua mikopo kwa ajili ya shughuli za kilimo na kurejesha.

"Kwa Kijiji cha Sole kuna mama ameanzisha mradi wa kuku na sasa wamefika 70, mwingine amejenga choo cha kisasa. Haya ni baadhi ya mafanikio makubwa. Pia wanapata elimu ya uhifadhi kwa shule za sekondari na msingi, tunawapeleka kwenda kutalii na kujifunza hifadhi za Udzungwa na Mikumi kutokana na namna wanavyofanya vizuri kweye mitihani hao, wanajifunza tabia za tembo na wakienda hifadhini wanaona," anasema.

Aidha, anasema kwenye mizinga changamoto ni kukosa nyuki kutokana na mazingira yaliyopo ambayo nyuki hajitengenezea chakula chao wenyewe na kusababisha mizinga kukosa asali.

Kwa mujibu wa Lim, miaka mitatu ijayo wataanzisha vikundi 16 katika vijiji nane ili kuendelea kuwasaidia wananchi na washirikisha kwa kila kitu ili viwe endelevu hata mradi utakapokwisha.

Mtaalamu wa nyuki wa kikundi cha Njokomoni, Ahemed Churi, anasema tembo walikuwa kero na kukwamisha kilima ndipo lakini ufumbuzi umepatikana baada ya STEP kuwaelimisha.

Wamefundisha kutengeneza uzio wa pilipili kwa kuweka vitambaa ambavyo akinusa anapiga chafya na kurudi alikotoka, lakini baadaye waligundua na kuanza kugeuka kinyumenyume kuingia mashambani.

"Tukabuni mradi wa nyuki ukiweka mizinga tembo hawataingia, kwa ufadhili wa hifadhi ya Udzungwa tulipata mizinga 20 na baadaye STEP wakatupatia 100 ambayo tumeiweka umbali wa mita moja, iliyounganishwa na nyaya ambayo tembo akija akitikisa nyuki wanatoka na kuwang'ata kisha wanakimbia," anasema.

Aidha, anasema mradi huo kwenye eneo la kilomita moja na mizinga 76 na yenye nyuki ni 19 pekee umekuwa na manufaa kwa kuwa zamani tembo walikuwa wanaingia kwenye mashamba lakini sasa wamewazuia.

Anasema mapato yao ni zaidi ya Sh. 300,000, akiomba wasaidiwe ili mradi uwe mkubwa ikiwamo kutambuliwa na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS), ili wafikishe bidhaa kwenye masoko ya nje na ndani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mang'ula A, Junior Mponela, anasema uelewa wa wananchi umeongezeka na kwamba kwa sasa wananufaika na miradi mbalimbali na wanyama sio tatizo kubwa kama ilivyokuwa awali ndio maana wanalima maeneo ambayo kwa miaka mingi hawakuyagusa.

Michael Mkaranga ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Sole, anasema awali tembo walikuwa wanaharibu mazao yao mara kwa mara lakini kwa sasa kuna nafuu kubwa na jamii inaona faida kwa kuwa kutokana na vikundi vinavyowapa mikopo na mbinu za kufukuza tembo ambazo zinawaletea faida kama kufuga nyuki.

Kaimu Mtendaji wa Kijiji cha Kanyenja, Mohamed Mohamed, anasema asilimia 75 ya mradi wa kufufua shoroba uko kijijini humo na kwamba serikali imefanya jambo kwa kuwa tembo walikuwa wanaharibu mazao kikubwa na sasa wanalima maeneo ambayo kwa miaka mingi hayakuguswa.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Hii ndiyo siri kisiwa cha maisha marefu

## • Hawali kilichosindikwa, nyama, juisi ya zabibu ndiyo maji yao

KUISHI miaka 100 ni jambo la kawaida sana kisiwani Ikaria. Mmoja kati ya wakazi watatu anaishi zaidi ya miaka 90. Kwa sababu hiyo, kisiwa hicho huitwa "ukanda wa bluu" jina linalomaanisha maeneo yenye maisha marefu yenye afya na ya kipekee duniani.

Sehemu nyingine zenye maisha marefu zaidi duniani ni pamoja na Sardinia nchini Italy, Okinawa huko Japan, Nicoya Costa Rica, Loma Linda Marekani na Ikaria, Ugiriki.

Makala hii inaangazia wakazi wa kisiwa kidogo cha Ikaria nchini Ugiriki wanaishi maisha marefu, kwa wastani wa miaka 10 zaidi ya watu wengine wa Ulaya Magharibi.

Na swali kubwa linabakia kuwa hili kuna siri gani katika kisiwa hiki cha maisha marefu?

Kwa mujibu wa mtandao wa euronews, mwaka 2021, wastani wa kuishi Ulaya Magharibi ni miaka 80.1, hivyo wakazi wa kisiwani hapo wanaishi zaidi ya miaka 90 na wengi hufikia 100+.

Inawezekana ni kuwapo kwa hewa safi, inaweza kuwa mboga safi zisizolimwa kwa mbolea na kemikali za viwandani na maziwa ya mbuzi?

Lakini pia kila sehemu ya kisiwa hicho ni kukavu, hivyo kutembea kunaweza kuchangia kujenga mwili wenye afya. Aidha, inaweza hata kuwa mionzi ya asili ya miamba ya mawe ya granite?

Lakini mkazi wa kisiwa cha Stamatis Moraitis anadhani anajua sababu ya maisha marefu ya watu wa kisiwa hiki.

"Ni kinywaji tunachotengeneza hapa," anasema, akiwa na glasi ya kinywaji juu meza ya jikoni kinachotokana na zabibu, majira ya asubuhi. "Kinywaji safi, hakuna kilichoongezwa ndani yake. Vinywaji vya kibiashara vimeongezwa vitu vingine visivyofaa kwa afya. Lakini hiki ni safi na tunakitengeneza sisi wenyewe."

Stamatis alisherehekea siku yake ya kuzaliwa akitimiza miaka 98, Januari 1 mwaka huu. Anasema ni mzee kuliko kinavyoeleza cheti chake cha kuzaliwa, kwamba alizaliwa Januari 1, 1915.

Nje ya nyumba yake kuna mizaituni, miti ya matunda na mizabibu, hutengeneza takribani lita 700 za juisi ya zabibu kwa mwaka.

"Unakunywa peke yako?" Anapoulizwa na BBC anasema hapana!"

Anasema na kushangazwa na swali na kueleza kuwa anakunywa na marafiki zake na kwamba hunywa zabibu na kupumzika na marafiki na familia.



Mzee aliyeishi karibu muongo mmoja akifurahia maisha wakati zabibu zikitajwa kuwa dawa ya kurefusha maisha kisiwani Ikaria. **PICHA: BBC**

### KUPONA SARATANI

Mzee huyo ni alama ya uponyaji kisiwani hapo, miaka 45 iliyopita, alipokuwa akiishi Marekani, aligunduliwa na saratani ya mapafu na kuambiwa ana miezi tisa pekee ya kuishi.

"Wakati huo ilikuwa ghali sana kufanya mazishi huko Marekani," anakumbuka. "Kwa hiyo nikamwambia mke wangu, 'nakwenda nyumbani kwetu Ikaria walikozikwa wazazi wangu.'

Ni hadithi ambayo ameisimulia mara nyingi, na hajachoka kuisimulia. "Niliwakuta marafiki zangu kijijini nilikozaliwa na tukaanza kunywa juisi ya zabibu. Nikifikiri nitakufa kwa amani."

"Kila siku tulikusanyika, tukanywa pamoja. Muda ulipita na nilihisi nguvu. Miezi tisa ilipita nilihisi afya zaidi, ikaja miezi 11 nayo ilipita - nilihisi niko vizuri. Sasa ni miaka 45 baadaye, bado niko hai," anasema.

Anaongeza: "Miaka michache iliyopita nilirudi Marekani na kujaribu kutafuta madaktari wangu. Lakini sikuweza kuwapata. Wote walikuwa wameshakufa." Anaeleza.

Kwa ujumla kuna hadithi nyingi kama hizi katika kisiwa hicho na miaka ya hivi karibuni wanasayansi na madaktari wamekwenda kwenye kisiwa ambacho si mbali sana na pwani ya Uturuki ili kujua ukweli wa maisha marefu.

### WANACHOGUNDUA

Daktari Bingwa wa magonjwa ya moyo wa Chuo Kikuu cha Athens, Dk. Christina Chrysohoou, ambaye aliwachunguza watu wa kisiwa hicho, anasema, 'wanakabiliwa na magonjwa ya saratani na matatizo ya moyo sawa na watu wengine, lakini wanayapata magonjwa hayo katika sehemu ya mwisho ya maisha yao, hayawahi kama ilivyo kwa wengine.

"Ikaria inatupa fursa ya kujifunza kwa nini watu hawa wanafurahia faida hizi, hatuwezi kuepuka magonjwa haya, lakini wanafanikiwa kudumisha ubora wa maisha yao kwa miaka mingi. Wastani wa umri wa ugonjwa wa moyo ni kati ya miaka 55 hadi 60. Lakini Ikaria watu hufikia hata miaka 70 kabla ya kupata tatizo hilo."

Pia kuna utafiti wa vinasaba unaowalinganisha watu wanaoishi kisiwani humo na waliozaliwa kisiwani humo lakini wakahama na hivyo kuishi maisha tofauti na ya watu ambao bado ni wazawa wanaishi Ikaria bila kuhama au kuondoka.

Anasema kukutana na baadhi ya wakazi wakongwe wa kisiwa hicho kutakufanya uvutiwe na maisha yao marefu.

Mama mwenye miaka zaidi ya 100, anasema meza ya chakula imejaa vyakula vya Ikaria. "Ni vitafunio," anasisitiza Voula, mke wa George Kassiotis mwenye umri wa miaka 102,"

Anapotoa kitambulisho chake kinachoonyesha tarehe yake ya kuzaliwa ni 1910 na kusimulia maisha yake ya utotoni.

Kwenye ukuta mmoja kuna picha yake akiwa katika kikosi cha wapanda farasi cha Ugiriki mwaka 1931 na kwamba alipigana nchini Italia dhidi ya Albania katika Vita vya Pili vya dunia, kisha akasaidia kujenga barabara ya kwanza ya chuma kisiwani humo kabla ya kustaafu mwaka wa 1970.

"Sili chakula kilichosindikwa, sivuti sigara, sina wasiwasi," George Kasiotis anasema. "Sina wasiwasi na kifo. Najua sote tutakufa."

### UTAMADUNI WAO

Aidha, inabainika kuwa kizazi cha vijana hujaribu kushika mila. Wanapata mlo mwingine nyumbani kwa Nikos Karoutsos, mmiliki wa mgahawa mwenye umri wa miaka 50, na kuona marafiki na familia nyingi wakija kwenye kwake kwa ajili ya vinywaji na chakula.

"Hatuna vilabu vya usiku wala sehemu za kucheza," anasema, huku watu wakigonganisha glasi zilizojaa juisi ya zabibu nyekundu kutoka kwenye chupa kubwa za plastiki. "Mlango uko wazi kila wakati, hakuna haja ya kupiga simu na kuuliza ikiwa uingie."

Wakiwa njiani kuelekea nyumbani wanampita Stamatis Moraitis mwenye umri wa miaka 98, akiwa anapanda ngazi hadi kwenye mzeituni wake mmoja ili kuchuma matunda.

"Nimefurahi bado ninaweza kufanya hivi," anasema huku akicheka. "Ninahisi afya zaidi hapa." Anaongeza.

**BBC SWAHILI**





# Daktari aonya jamii kuhusisha ugonjwa selimundu, tiba asili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Damu wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), Stellah Malangahe, ameitaka jamii kutohusisha ugonjwa wa selimundu na tiba za kienyeji.

Badala yake amewataka kuwapeleka wagonjwa katika vituo vya afya kwa ajili ya kupata vipimo na matibabu stahiki.

Aidha, alisema hivi sasa serikali inapeleka timu za wataalamu katika hospitali za wilaya kwa lengo la kusaidia utoaji huduma katika maeneo mbalimbali kwa wagonjwa wenye tatizo hilo na matatizo mengine ya kiafya.

Stellah alisema serikali kupitia wataalamu wa afya inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ugonjwa wa selimundu ili kuhakikisha wanatambua na kuelewa dalili za ugonjwa huo ikiwamo kuwashawishi kuhudhuria katika vituo mbalimbali vya afya ili waweze kupatiwa matibabu.

"Kuuzuia ugonjwa wa sikoseli inawezekana hivyo jamii inapoona mtoto anadalili hizo wamepelekwa hospitali wasikimbilie kumtibu kienyeji kabla ya kukutana na wataalamu wa afya," alisema.

Akizungumza kuhusu huduma ya upandikizaji uloto kwa watoto wenye tatizo la sikoseli alisema hadi sasa wamepandikiza watoto wanne, kwamba kati ya hao watatu wameruhusiwa huku mmoja akiendelea na matibabu.

Alisema idadi hiyo ya wagonjwa waliopandikizwa uloto hospitalini hapo afya zao zinazidi kuimarika kila siku na kuongeza kuwa tatizo hilo linatibika kama mgonjwa atawahi kwenda katika vituo vya afya kupata matibabu.

"Wagonjwa watatu katika ya wanne ambao wamepandikizwa uloto wameruhusiwa na afya zao zimeimarika na mwingine anaendelea na matibabu ili afya yake imarike na kuruhusiwa kutoka hospitalini hapo," alisema Dk. Malangahe.

Malangahe alisema jamii inapaswa kujitokeza kupeleka watoto katika vituo vya afya kukutana na wataalamu wa sekta hiyo ili kubaini kama wanashida hiyo ili waweze kuwapatia huduma ya kwanza.

"Jamii inapaswa kuwa makini kuangalia afya za watoto pale wanapoona kuna changamoto au dalili za tatizo la sikoseli (selimundu) wampeleke katika kituo cha afya au hospitali ili aweze kupatiwa matibabu ya awali kabla ya kupewa rufani kwa ajili ya matibabu zaidi atakapogundulika ana tatizo la selimundu," alisema Dk. Malangahe.

Alisema BMH imeanzisha kutoa huduma hiyo ili kuunga mkono jitihada za serikali za kupunguza au kutokomeza kabisa ugonjwa wa selimundu hapa nchini kwa watoto ambao ni taifa la kesho.

Vile vile, alisema Tanzania ni nchi ya nne duniani kwa kuwa na wagonjwa wa selimundu, hivyo ni vema jamii ikajua hilo na kuzingatia maelekezo wanayopewa na wataalamu wa afya ili kudhibiti ugonjwa huo.



Mafundi wakiweka lami kwenye Barabara ya Kilwa, eneo la Mbagala Zakhiem jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bil.437/- kutekeleza miradi ya maendeleo Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIKA kipindi cha miaka miwili serikali imeupatia Mkoa wa Singida Sh. bilioni 437.683 sawa na ongezeko la asilimia 252.8 ya Sh. bilioni 124 zilizotolewa mwaka 2019/2020 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema hayo jana wakati akitoa taarifa ya mafanikio ya serikali kuanzia Machi 2021 hadi Juni 2023 wakati wa mkutano wa hadhara wa Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

Mkutano huo ulihusu utoaji elimu ya makubaliano ya Serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu uendeshaji wa bandari uliowashirikisha wananchi kutoka mikoa ya Singida, Dodoma na Tabora.

Alisema katika kipindi hicho utekelezaji wa miradi ya umeme zilitolewa Sh.bilioni 109.6 ambazo zimewezesha vijiji 341 kati 441 sawa na asilimia 77.32 vimeunganishwa huduma ya umeme katika gridi ya taifa hadi kufikia Machi 2021.

Serukamba alisema katika wateja wapya 19,223 waliounganishiwa umeme ni pamoja na shule 287, visima vya maji 23, viwanda vidogo 76, migodi ya madini ya dhahabu 5, misikiti 43, makanisa 60, mahakama 2 na vituo vya kibiashara 102.

Kuhusu mpango wa TASAF, alisema hadi kufikia Juni 2023 utekelezaji umefika kwenye vijiji vyote 441 vya Mkoa wa Singida na mitaa 53 ambapo walengwa wamepokea ruzuku ya masharti ya ajira za muda Sh. bilioni 14.317 zilizotolewa na serikali.

Serukamba alisema katika sekta ya afya kwa kipindi hicho zimetolewa Sh.bilioni 47.272, elimu Sh. bilioni 56.223, sekta ya uzalishaji serikali imetoa Sh.bilioni 44.386, maji Sh.bilioni 14.635.

Aliongeza kuwa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), imesaidia ongezeko la upatikanaji wa maji kutoka asilimia 57.9 mwaka 2020/2021 na kufikia asilimia 67.7 Juni 2023 sawa na wakazi 1,109,220 waishio vijijini.

Alisema Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) Mkoa wa Singida uliopewa Sh.bilioni 52.033 ambazo zimeweza kutumika katika ujenzi wa barabara mbalimbali zenye urefu wa kilometa 1,718.31 zinazohudumiwa na wakala huyo.

# Mavunde awashukia askari mgambo wanaopoka bidhaa

**Na Gloria Mganza,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde amewataka askari mgambo wa Jiji hilo kutotumia nguvu na mabavu kwa kuwanyang'anya bidhaa zao badala yake wawaelekeze kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mavunde, aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati akisikiliza kero mbalimbali za wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Majengo.

Katika mkutano huo malalamiko makubwa yalilenga katika namna ambayo mgambo wa Jiji wamekuwa wakitumia mabavu katika kushughulika na wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga.

"Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha kujenga soko kubwa la wamachinga hapa Dodoma kama ishara ya kuthamini na kuheshimu shughuli hizi za wafanyabiashara wadogo, lazima na sisi wa ngazi ya chini ya uongozi tuishi katika maono ya ya Rais.

"Nimesikia kilio chenu juu ya changamoto hii ya askari wa Jiji na tayari nilishamuita Mwanasheria wa Jiji pamoja kiongozi wa askari hawa kuhakikisha wanatumia utaratibu mzuri ambao hauwezi kuleta athari kwa wafanyabiashara wadogo," alisema Mavunde.

Alisema ni lazima kuwaheshimu sana kinamama wanaofanya biashara ya kubeba mabeseni pamoja na kinababa wanaozunguka kutwa nzima wakiwa na bidhaa kujitafutia riziki. "Lakini pia ni waombe na ninyi wafanyabiashara wadogo kufuata sheria na maelekezo yanayotolewa ili kutoingia kwenye sintofahamu na hawa askari wa Jiji," alisema Mavunde.

Katika mkutano huo pia mbunge huyo aligawa viti 200 kwa kikundi cha vijana cha Majengo asili kama sehemu ya uwezeshwaji kiuchumi kupitia mradi wa ukodishaji viti.

Mkutano huo wa hadhara uliihudhuriwa pia na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Charles Mamba, Katibu wa CCM Wilaya, Sofia Kibaba na wajumbe wa kamati ya siasa ya wilaya.





# Mtambo wa kuchoronga visima vya maji watelekezwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MTAMBO wa kuchorongea visima vya maji uliotolewa na serikali kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji mkoani Mbeya, umetelekezwa kwa zaidi ya miezi miwili wilayani Chunya huku wilaya hiyo ikikabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma.

Kutelekezwa kwa mtambo huo kulibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa iliyokuwa na lengo la kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Kwenye kikao cha kamati hiyo ya siasa na madiwani wa Halmashauri ya Chunya iliibuka hoja ya uhaba wa maji kwenye maeneo mengi ya wilaya hiyo, huku madiwani wakihoji kuhusu mtambo wa kuchorongea visima.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi Ismail Nassoro Ismail, alikiri kutelekezwa kwa mtambo huo huku akidai tatizo lipo kwenye mfumo wa uendeshaji. Alisema mtambo huo unasimamiwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa nchini (DDCA) ambacho kipo chini ya RUWASA na kwamba wataalamu wa kuendesha mitambo hiyo wanaishi jijini Dar es Salaam.

Alisema ofisi yake ilishawalipa DDCA Sh. milioni 280 kwa ajili ya kuchimba visima 14 wilayani humo lakini kabla ya kutelekeza mitambo hiyo walichimba visima sita pekee.

Alisema wamekuwa wakiwafuatilia kwa kuandika barua na kupiga simu lakini bado wamekuwa wazito kujitokeza kwenda kuchimba visima hivyo, huku muda wa mtambo huo kufanya kazi wilayani humo ukiwa unaelekea ukingoni. "Awali walichimba visima vinne wakaondoka tulisumbuana mpaka nikalazimika kuwasiliana na mbunge wa jimbo hili na alipohoji bungeni kesho yake walikuja wakachimba visima viwili ndipo wakaja wakaegesha mitambo hapa na hawajaonekana tena," alisema Mhandisi Ismail.

Alisema kwa sasa wanasingizia mfumo wa malipo kufungwa lakini tatizo lilikuwapo hata kabla mfumo huo haujafungwa na hivyo akawaomba viongozi wa chama kuwasaidia kufuatilia.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka alisema Wilaya ya Chunya inakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji kwa wananchi na hivyo inahitajika jitihada zaidi kutumia mtambo huo pamoja na kutafuta vyanzo mbadala vya maji.

Alisema kwa sasa hali ya upatikanaji wa maji iko chini ya asilimia 50 huku miradi mingi ikisuasua na kwamba suluhisho la kudumu itakuwa ni utekelezaji wa mradi wa miji 28 ambao wilaya hiyo ni miongoni mwa wanufaika.

"Chanzo cha maji ambacho kitakuwa suluhisho ni cha Mto Gwaziva maana kwa hapa mjini visima vya kuchimba hatupati maji, walijaribu kuchoronga kisima kimoja wakafika zaidi ya mita 200 lakini hawakupata maji," alisema Kasaka.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka alisema mtambo huo unatakiwa kuondolewa wilayani humo kabla ya Oktoba Mosi na kupelekwa katika wilaya nyingine.

Alisema serikali ya mkoa iliamua kuanza na Chunya kutokana na kuwa ndiyo wilaya inayoongoza kwa kuwa na tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo ya maji.



Baadhi ya wafanyakazi wa mgodi wa Barrick Bulyanhulu uliopo mkoani Shinyanga wakipata mawaidha ya kulinda afya zao kabla ya kuanza kukimbia mbio za uzinduzi wa kampeni maalumu ya kutokomeza ugonjwa wa malaria uliofanyika mgodini hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waiangukia serikali kusaidiwa kupata maji ya bomba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kuwasaidia kutatua kero ya maji kwenye maeneo yao wakidai kuwa hawajawahi kupata maji ya bomba.

Wamesema wamekuwa wakilazimika kutumia maji ya kwenye makorongo na vijito vidogo ambavyo wakati wa kiangazi kikali huwa vinakauka.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ambaye alifika kwenye kata hiyo kwa lengo la kusikiliza kero za wananchi.

Mmoja wa wananchi hao, Zebedayo Shila, alisema wanapata shida zaidi wakati wa kiangazi ambapo huwa wanalazimika kwenda kuchota umbali wa zaidi ya kilomita tatu. Alisema katika maeneo hayo kuna vyanzo vingi vya maji ambavyo vinaweza vikasaidia kuwasogezea huduma ya maji kwenye maeneo yao.

Alisema: "Sisi hapa kama unavyoona hata wanafunzi wa shule yetu ya msingi wanakwenda kuchota maji kule chini, huku kuna mito inapita ambayo tunaweza tukasaidiwa kupata maji ya bomba".

Mbunge Njeza alikiri eneo hilo kukabiliwa na tatizo la uhaba wa maji na kwamba atawasiliana na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kutatua kero hiyo ambayo ni ya muda mrefu.

Alisema eneo hilo ni miongoni mwa maeneo yenye vyanzo vingi vya maji na hivyo hakuna sababu ya wananchi kuendelea kupata shida ya upatikanaji wa huduma hiyo muhimu.

# Maandalizi Sikukuu ya Wakulima yazidi kunoga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAANDALIZI kwa ajili ya maonyesho ya kimataifa ya wakulima (Nane nane) yatakayofanyika katika Uwanja wa John Mwakangale mkoani Mbeya yanaendelea, kwamba miundombinu mbalimbali inaendelea kuboreshwa.

Vikao mbalimbali vya wadau pamoja na serikali vinaendelea kwa ajili ya kuhakikisha maonyesho hayo yanakuwa na tija kwa wananchi hasa kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mwishoni mwa wiki kilifanyika kikao cha pili cha maandalizi ya maonyesho hayo ambacho kiliwashirikisha viongozi wa serikali kutoka katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na maofisa kutoka katika Wizara ya Kilimo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliwataka washiriki wa maonyesho hayo kuandaa mazingira bora ya wakulima kujifunza mbinu bora za kilimo ili wakazitumie kwenye maeneo yao na kuongeza uzalishaji.

Alisema wataalamu wanatakiwa kutumia lugha rahisi na kueleweka kwenye utoaji wa elimu kwa wananchi ili kuepuka kuwachanganya badala ya kuwasaidia.

Alisema endapo wakulima watashindwa kujifunza mbinu hizo za kisasa maonyesho hayo hayatakuwa na tija kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na taifa kwa maelezo kuwa lengo la maonyesho ni kuleta mabadiliko kwa wakulima.

Alisema: "Washiriki wa maonyesho watakaotuletea teknolojia wanatakiwa kuandaa mazingira ambayo yatakuwa rafiki kwa wakulima wetu kujifunza vizuri, tusipofanya hivyo basi hatutapata tija kabisa kwa hiyo tuanze kujiandaa."

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, alisema maandalizi ya maonyesho hayo yamekamilika kwa zaidi ya asilimia 80 na kwamba maeneo yaliyobakia ni madogo madogo.

Alisema maonyesho hayo kwa mwaka huu yatakuwa tofauti kutokana na kuwapo kwa wageni kutoka katika mataifa mbalimbali duniani ambao wamealikwa kwa ajili ya kushiriki.

Alisema miaka yote maonyesho hayo yalikuwa yanafanyika kikanda na kitaifa lakini kwa mwaka huu ni maonyesho ya kimataifa.

Aliwataka wananchi kujitokeza kwenda kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo ili waongeze tija kwenye uzalishaji wa mazao wanayolima pamoja na kupata masoko kwa ajili ya mazao hayo.

"Tutapata wageni kutoka mataifa mbalimbali, wengine wataleta teknolojia za kilimo, wengine ni wanunuzi wa mazao na wengine watakuja kujifunza teknolojia zetu, kwa hiyo sisi tunawakaribisha wananchi wetu wajitokeze kwa wingi," alisema Chimagu.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Njombe, Ayoub Mdeme, alisema mikoa ya Nyanda za Juu kusini ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na hivyo ni muhimu wakulima kupatiwa elimu ili waendelee kuzalisha.

Aliwataka wakulima kuwa na utamaduni wa kujifunza vitu vipya kutoka kwa watu wengine ili kuboresha mbinu za uzalishaji, huku akisisitiza kuwa kwa sasa dunia inakabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaweza kuathiri uzalishaji.



# Wanaosoma utalii watakiwa kuwa na maadili, ukarimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, amewataka vijana wanaosoma fani ya kuhudumia watalii kufuata maadili, kuwa wakarimu kwa watu wanaowahudumia.

Aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya kwanza ya wanafunzi wa Chuo cha Zenj Center of Excellence for Tourism Vocational yaliofanyika Zanzibar.

Waziri Simai alisema miongoni mwa juhudi za Serikali ya Zanzibar ni kuwekeza katika elimu kupitia fani mbalimbali ikiwamo ya utalii ili vijana waweze kuajiriwa na kujiajiri katika sekta hiyo.

Hivyo, aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kufahamu kuwa kazi yoyote lazima iongozwe na maadili kwa mujibu wa fani husika hivyo wakati umefika kwa vijana hao kujitahidi na kuwa weledi katika kazi zao hizo.

Waziri Simai alisema katika kufikia malengo ya chuo hicho wizara yake inazungumza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kukiunganisha na Chuo cha Utalii Maruhubi ili wanafunzi wa chuo hicho kupata uzoefu zaidi katika mambo ya utalii.

Alisema serikali inathamini wawekezaji wanaofika kuwekeza katika mambo ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa hoteli ili kuongeza pato la taifa na nchi kupata maendeleo. Alisema hivi sasa katika soko la dunia ajira zimekuwa ngumu hivyo aliwataka wahitimu hao kufanya kazi usiku na mchana ili kuendana na ushindani huo.

"Serikali ya Zanzibar haifurahii hata kidogo kuona vijana wa Zanzibar wamesomea fani ya utalii lakini hawako vizuri katika ufanyaji wao wa kazi pale wanapoajiriwa katika hoteli za kitalii," alisema.

Naye Mwenyekiti wa chuo hicho, Taufiki Salum Turky, alisema lengo la kuanzishwa kwa chuo hicho ni kuwaendeleza vijana kupata ajira baada ya wimbi kubwa la vijana hasa wakati nchi ilipokubwa na janga la ugonjwa wa virusi vya corona. Alisema chuo hicho kwa mara ya kwanza kinatoa wahitimu 24 kwa ngazi ya cheti lakini vijana hao wamebobea katika fani ya utalii na kuwaunganisha katika hoteli za kitalii ili kuajiriwa.

Aidha, alisema licha ya vijana hao kupatiwa mafunzo yanayohusu utalii lakini wamelelewa katika maadili ya kizanzibari na wako tayari kufanya kazi sehemu yoyote.

Mkurugenzi wa chuo hicho, Yves Montel, alisema katika kufikia malengo kwa taaluma hiyo kwa vijana tayari washafanya mazungumzo na Serikali ya Ufaransa ili kujenga chuo kingine kitakachotoa fani kama hiyo.

Alisema vijana wa Zanzibar wanauwezo wa kufanya kazi sehemu yoyote katika fani ya utalii kwa vile wamepatiwa mafunzo mazuri na walimu wenye uwezo.

Aidha, alisema wataendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mipango ya maendeleo ikiwamo katika sekta ya utalii.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi (kulia) na Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Canada, Harjit Sajjan (wa pili kulia), wakiwa wanataniana na Mwasiti Ramadhani mwenye ulemavu wa macho na mmoja wa wateja wakuu wa kitengo cha uzazi cha CCBRT katika wodi ya wazazi ambaye amejifungua salama mtoto wa kiume. Waziri alitembelea CCBRT mwishoni mwa wiki kujionea kazi ya kugusa maisha ya watu inavyofanywa na hospitali hiyo. Wengine ni maofisa kutoka Hospitali ya CCBRT na Canada. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sera ya Jinsia yasaidia ushiriki wanawake katika uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UUNDWAJI wa sera ya jinsia na ushirikishwaji wa jamii ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar umesaidia kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi.

Katika sera hiyo mikakati mbalimbali imeainishwa ili kufikia malengo ikiwamo kuweka mifumo itakayohakikisha usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa kijamii katika hatua zote za uchaguzi.

Hayo yalisemwa na Maulid kutoka Tume ya Uchaguzi Zanzibar wakati akiwasilisha maada ya wanawake na uongozi kwa wanasiasa wanawake wanaotarajia kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar.

Alisema sera hiyo imeundwa baada ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar kupata maoni ya wadau wa uchaguzi kuhusu ushirikishwaji wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika harakati za uchaguzi wa Zanzibar.

Aidha, alisema Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Namba 4 ya Mwaka 2018 na sera ya jinsia na ushirikishwaji wa jamii ya tume hiyo iliyoazishwa mwaka 2025 ni miongoni mwa nyaraka muhimu za kisheria zinazotumika na tume katika kutekeleza majukumu yake.

Alisema Kifungu cha 35 cha Sheria hiyo kinatoa fursa kwa mwanamke kushiriki kupiga kura kwa vile kimebainisha watu wenye haki ya kupiga kura ambao ni kwa kila mtu aliyeandikishwa katika daftari kuwa mpiga kura.

"Hii inamaana raia wote wa kike na wakiume wenye sifa za kuandikishwa kupiga kura wanayo haki ya kupiga kura kinyume na uchaguzi wa awali wa Zanzibar wa mwaka 1957 ni wanaume pekee ndiyo waliruhusiwa kupiga kura," alisema.

Vilevile alisema Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar imetoa fursa kwa mwanamke kushiriki kugombea uongozi kwa nafasi za kisiasa ikiwemo urais, uwakilishi, ubunge na udiwani ili mradi awe na sifa maalumu zilizoainishwa katika Katiba ya Zanzibar. Akizungumza katika mafunzo hayo, Mratibu wa mradi wa nafasi za uongozi kwa wanawake kutoka TAMWA, Mariam Ame Chuom, aliwataka wanawake kuwa wajasiri na kujitayarisha kiongozi bila kuogopa changamoto zinazowakabili wanapoingia katika uongozi ili kuongeza ushiriki wao kwenye vyombo vya maamuzi.

Alisema idadi ndogo ya wanawake katika vyombo vya maamuzi na michakato ya kidemokrasia umekuwa ukijidhihirisha katika uchaguzi zinazofanyika nchini kila baada ya miaka mitano ambapo wanawake hupata nafasi chache.

Alisema jambo hilo linaweza kuwa kikwazo kwa Tanzania kutokomeza umaskini na kuimarisha demokrasia inayowapa wananchi haki ya kuchagua kiongozi wamtakae.

# ACT-Wazalendo yasisitiza amani, mahitaji ya wananchi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT -Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar inahitaji kuingia katika mageuzi yakayofanywa kwa kuzingatia amani, kuzingatia mahitaji ya wananchi.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, ameyasema hayo Wilaya ya Mjini Unguja wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara wa chama hicho.

Alisema kwamba hatua hiyo ni muhimu na itasaidia nchi kuendeshwa kwa mujibu wa maono ya viongozi wa chama na wananchi wanavyotaka.

Alisema kwamba hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kuendelea na kupiga hatua iwapo wananchi hawana uwezo na mamlaka ya kuwachagua na kuwawajibisha viongozi wao waliowachagua.

"Ni busara viongozi wa serikali kuwa na utaratibu wa kujisema wenyewe jambo litakalosaidia kuwapo utamaduni wa utakaojengwa ndani ya chama kutimiza ahadi walizoziweka kwa wananchi kwa kuichunga serikali," alisema.

Aidha, alisema ni jambo muhimu kuwapo kwa muungano wenye kuzingatia haki katika ushirikiano wa kusimamia masuala mbali mbali yanayofanywa ikiwa ni pamoja na kuwepo uwezo wa kupanga kodi kwa mujibu wa hali ya uchumi wa Zanzibar bila kuwepo vizuizi.

Akizungumzia kuhusu rasilimali ya mafuta na gesi asilia alisema mfumo wa muungano uliopo Zanzibar haina mamlaka ya kisheria kuchimba mafuta kwa kuwa sheria inayosimamia rasilimali hiyo ndivyo inavyoeleza hadi sasa.

Othman aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na kushikamana kwa kukiunga mkono chama hicho kwa kuwa kina maono ya kutafuta maendeleo ya kweli kwa wananchi wa Zanzibar.

Aidha, aliwataka wananchi wote ambao hawana kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi kuhakikisha kwamba wanafanya juhudi za kujiandikisha ili waweze kupata haki yao hiyo muhimu ambayo inaambatana na suala la kuwa mpigakura.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Nassor Ahmed Mazuri, alisema wananchi wanapaswa kushirikiana kukiunga mkono chama hicho kuendelea kuwa chama imara ambacho kimejiimarisha katika kuleta mageuzi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAMWELI BASHAGHEDA SURUMBU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T299DBD** aina ya **Toyota Noah,** Chasis namba **SR400224181,** Engine namba **3S7942814** Kwa yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA YA POLISI: **MAN/HAN/RB/245097/2023**

### KUPOTEA KWA PASSPORT



**VALENCE TUMBO MASSAWE** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 018694** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 5/4/2018. Tarehe ya kuisha matumizi ni 4/4/2028. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/234064/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la madai 32, 2023**
**Jina la Mdai Richard Godson Mbaga**
**Jina la Mdaiwa Bahati John Mwahingile**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa: Bahati John Mwahingile**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai )**

Mdai ameleta madai ya talaka dhidi yako.Fika Mahakamani kujibu madai hayo
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 26 mwezi 07 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21 mwezi 07 Mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MOSHI – MJINI

### KUFUNGA KAMPUNI

**MKURUGENZI WA KAMPUNI YA KOFIA MBAYA'S R BUSINESS CONSULTANTS. YENYE USAJILI NAMBA 162915096 ANAPENDA KUWATANGAZIA KUWA KAMPUNI INAFUNGWA KWA SABABU YA KUSHINDWA KUJIENDESHA**

**IMETOLEWA NA:**

**GODFREY GERVAS HEBUKA**

**MKURUGENZI**
**KOFIA MBAYA'S R BUSINESS CONSULTANTS COMPANY LIMITED.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha BULELA Mkoa GEITA**
**Shauri la madai/Ndoa Na. 15/2023**
**Jina la mdai EVER ALEX**
**Jina la mdaiwa JONAM WILLIAM JOSIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa**
**JONAM WILLIAM JOSIA**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai)**

**KUJIBU MADAI YA TSH 7,000,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 2 mwezi 8 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17 mwezi 7 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
BULELA_GEITA.

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 362 CJV – BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/822435/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......69/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: CHRISTINA F KUNAMBI wa MSAMSAVU "B"**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA FABIAN JORDAN KUNAMBI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 02 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 07 mwaka 2023
G.A.NG'ITU

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NAHUMU LUNOSO MSIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 300 CFF** aina ya **FEKON**. Chassis namba **LDAPAJOB3KG03109.** Engine namba **157FMI219F0319.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/243926/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MIKESE**
**MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA.29/2023**
**MDAI: DENIS LUWANDA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: GIBSON ZABLON BUZOYA**
**KWA: GIBSON ZABLON BUZOYA**
**DAR ES SALAAM**
**OMBI LA MDAI: DENIS LUWANDA, MADAI YA PESA TSHS.220, 000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika Shauri tajwa hapo juu bila kukosa,Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 26 mwezi 7 mwaka 2023 saa2:30 Asubuhi.
ANGALIA ALAMA: kuhudhuria/Haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama imethibitisha kama umepokea/Mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/Mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi 07 mwaka2023.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MIKESE
MOROGORO

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
MIKESE

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni IndustRial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mob: +255 - 0677020701***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Mkuu wa Kitengo cha CRDB Wakala, Ericky Willy (wa pili kushoto), akimkabidhi mshindi wa mwezi wa tano wa kampeni ya "CRDB Wakala 10 na Kitu", Joshua Lembeli Loketa, kadi ya Bajaj baada ya kuongoza kwa idadi ya miamala katika kampeni hiyo. Wengine pichani ni baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya CRDB, pamoja na wake wa mshindi huyo.

# Mfugaji aibuka mshindi bajaji kampeni ya CRDB

**Na Mwandishi Wetu, KILOSA**

KATIKA Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Joshua Loketa, amesimama huku akitabasamu akiwa ameshikilia funguo za bajaji yake mpya.

Akiwa CRDB Wakala, Joshua ameibuka mshindi katika kampeni inayoendelea ya CRDB Wakala '10 na Kitu', ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 10.

Furaha ya Joshua inaonekana wazi wakati akitoa shukrani zake kwa benki hiyo kwa zawadi hiyo ya bajaji, akieleza namna itakavyosaidia kwa kiasi kikubwa maisha yake, hasa katika kuwasafirisha watoto wake shuleni. Awali, Joshua alilazimika kutenga Sh. 60,000 kila mwezi kwa ajili ya gharama zao za usafiri.

Lakini safari ya Joshua na CRDB Wakala ni zaidi ya kushinda zawadi. Ana hadithi ya kipekee ambayo inamtofautisha na wengine. Joshua ni mfugaji, pia mhasibu wa kampuni ya ulinzi. Kilichomsukuma kuwa CRDB Wakala ni fursa iliyotolewa na Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), Chuo cha Afya na jamii ya Wamasai ambayo yeye ni kiongozi.

Kwa ujuzi wake wa kibiashara, Joshua aliona uwezekano wa kutoa huduma za kifedha kwa wafanyakazi wa miradi ya SGR, wafanyakazi na wanafunzi wa Kituo cha Afya pamoja na jamii. Aliamini katika kutoa huduma bora kwa wateja na hii inamtofautisha na wengine.

Weledi wake katika utoaji huduma na kufanya kazi unaonekana katika idadi ya wateja ambao anawapatia huduma - tayari amefungua zaidi ya akaunti 1,000 katika vituo 12 vya mradi wa SGR. Lakini hana mpango wa kuishia hapo. Maono yake ni kuongeza mtaji na kupanua biashara yake, kuongeza wateja wapya na kufungua ofisi nyingi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro.

Kamisheni anazopata kwa kuwa CRDB Wakala haijamwezesha Joshua tu kutimiza mahitaji muhimu ya familia yake bali pia imemjengea heshima katika jamii na miongoni mwa mawakala wengine. Amekuwa mfano wa kuigwa na wengi wanaotamani kufikia ndoto zao kwa bidii na kujituma.

Kampeni ya '10 na Kitu' inapoendelea, hadithi za mafanikio na mabadiliko zinaendelea kujitokeza. Safari yake ni mfano mmoja wa mapinduzi ambayo CRDB wakala imekuwa nayo kwa maisha ya mawakala na jamii wanazohudumia.

Kwa kila huduma na akaunti inayofunguliwa, Benki ya CRDB inachukua hatua nyingine kuelekea dira yake ya kukuza ushirikishwaji wa kifedha na kuboresha maisha ya Watanzania.

Ikiwa na mtandao mpana zaidi wa mawakala zaidi ya 30,000, Benki ya CRDB inaongoza kwa uwakala wa benki nchini na inashikilia nafasi tatu kwa ukubwa Afrika Mashariki. Mtandao huo mkubwa unatoa huduma kwa zaidi ya Watanzania milioni tatu kila mwezi. Ripoti za utendaji zinaonyesha zaidi ya miamala milioni 80 yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 50 hufanyika.

Mafanikio hayo yasingewezekana bila jitihada za CRDB Wakala na uhusiano thabiti walioujenga na jamii wanazozipa huduma. Kwa kuadhimisha miaka 10 ya CRDB Wakala, benki ilizindua kampeni ya miezi minne yenye lengo la kuongeza kasi ya ufikishaji wa huduma za benki kwa wananchi walio wengi zaidi.

# TANAPA: Sh. milioni tano unampa mnyama jina lako

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limeanzisha utaratibu maalum wa kuwezesha watu wanaotaka baadhi ya wanyama waitwe majina yao, kufanya hivyo lakini kwa malipo ya Sh. milioni tano.

Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, Willium Mwakilema, aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya TANAPA na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Alisema kumekuwa na utaratibu wa wanyamapori mbalimbali walioko katika hifadhi za taifa kupatiwa majina ya watu kama vile Faru John na mengine mengi, hivyo kama kuna mtu ambaye anataka jina lake apatiwe mnyama, gharama ni Sh. milioni tano.

"Tumeanzisha utaratibu wa kuwapa majina baadhi ya wanyama lakini sio bure. Na hawa wanyama sio wote labda kama umesema kuwa unampenda sana fisi unataka huyo fisi awe na jina lako," alisema na kuongeza:

"Kila mtu anaweza kumpatia mnyama jina lake ili alitumie kama utambulisho wake hifadhini, hivyo niwakaribishe watu wote ambao wangependa majina yao wapatiwe wanyama wetu katika hifadhi zetu ikiwa ni sehemu ya kuwalinda."

Akizungumzia mikakati ya TANAPA katika kulinda wanyama katika hifadhi za taifa, Mwakilema alisema hivi sasa wanafanya ulinzi na doria kutumia askari wao kwa saa 24 ili kulinda rasilimali hiyo ya taifa isipotee.

"Wanyama kama faru walipotea kabisa katika miaka ya nyuma, lakini kutokana na maajabu ya uumbaji wa Mungu mwaka 1993, walioneka faru jike wawili katika Hifadhi ya Serengeti na baada ya muda dume mmoja aliungana nao na hadi sasa wamezaliana na kufika 40 ambao tunawalinda usiku na mchana kwani pembe yao ile thamani yake ni zaidi ya dhahabu," alisema.

Kamishna Mwakilema alisema kwa kutumia askari wa wanyamapori pamoja na mbinu za kiteknolojia, wanafunga vifaa maalum wanyama hao ili waonekane kila wanakokwenda na hata pale wanapokuwa katika maeneo hatarishi.

Pia alisema faru hao wamekuwa kivutio kikubwa cha watalii nchini, hivyo hawana budi kutumia rasilimali zao zote kuwalinda kutoka kwa majangili ili waendelee kuliingizia taifa mapato.

Alisema mweleko wa TANAPA katika mwaka huu wa fedha wamepanga kukusanya mapato yatokanayo na vivutio vya utalii Sh. bilioni 343.8.

"Katika mwaka wa fedha uliloishia Juni 30, 2023, tulipanga kukusanya mapato ya Sh. bilioni 300 lakini kutokana na jitihada zizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kuitangaza nchi ndani na nje na kupungua kwa makali ya UVIKO-19 tulikusanya Sh. bilioni 337 kiasi ambacho kilivunja rekodi ambayo hatujawahi kukusanya hapo awali," alisema.

Vilevile, alisema TANAPA linaendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali katika hifadhi zote kwa msaada wa serikali pamoja na wadau wengine ikiwamo Benki ya Dunia (WB).

"Hifadhi ambazo zina watalii wengi hivi sasa ni zile za Ukanda wa Kaskazini, lakini lengo letu ni kuimarisha pia za kanda zingine ambazo ni pamoja na ile ya Mikumi, Nyerere, Sadani, Mkomazi na Ruaha ili kuongeza idadi ya watalii kufikia agizo la Ilani ya uchaguzi linalotaka ifikapo mwaka 2025/26 kuwa na watalii milioni tano na mapato yatokanayo na utalii dola za Marekani bilioni sita," alisema.

Alisema mikakati mingine ni kulinda mito minne ambayo inatoka nje ya hifadhi za taifa ili kulinda ikolojia na kuwaondoa katika hatari wanyama ya kukosa maji endapo itakauka kutokana na kuathiriwa na shughuli za kibinadamu.

HABARI MICHEZO

# MKANDALA, NG'ONDYA WATUA KAGERA SUGAR, IKIACHA SABA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI aliyepewa 'thank you' na Azam FC, Cleophace Mkandala, ametua Kagera Sugar na kutia saini mkataba wa miaka miwili, huku klabu hiyo ikitangaza kuachana na jumla ya wachezaji saba.

Klabu hiyo pia imepata saini ya mchezaji wa Mbeya City, Richardson Ng'ondya, ambaye ataanza kuitumikia kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Kagera Sugar imeanza kukisuka kikosi chake baada ya kutofanya vema msimu uliomalizika, ikimaliza ligi na pointi 35, ikishika nafasi ya 11, lakini ilikuwa moja ya timu ambazo hazikuwa na uhakika wa kubaki na hatihati ya kucheza mechi za 'play off' hadi ligi ilipomalizika.

Mkandala alimaliza mkataba wake na Azam ambayo ilimsajili kutoka Dodoma Jiji misimu miwili iliyopita, iliipiga kumbo Simba kumwania mchezaji huyo.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza kuwa usajili wa wachezaji hao ni mahususi kwa ajili ya kukitengeneza kikosi hicho ili kiwe cha kutisha kuelekea msimu ujao wa ligi.

Imeeleza bado inaendelea na mchakato wa usajili huku ikiwa imeacha baadhi ya wachezaji ambao hawawahitaji tena kuendelea nao na ambao mikataba yao imemalizika na haitowaongeza.

Wachezaji waliopewa 'thank you' na Kagera Sugar ni Jackson Kibirige, Laurent Alfred, Yusuph Mhilu, Abeid Athumani, Yusuph Dunia, Erick Mwijage na Meshack Mwamita.

KAZI IMEANZA ...



Kipa mpya wa Simba, Mbrazili Jefferson Luis, akiwa mazoezini na timu yake hiyo mpya kambini nchini Uturuki juzi. **PICHA: SIMBA**

# Kaze apewa mwaka Namungo

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Namungo imemtangaza Kocha wa Msaidizi wa zamani wa Yanga, Cedric Kaze, kuwa Kocha Mkuu na atakinoa kikosi hicho kuelekea msimu ujao wa mashindano.

Akizungumza na gazeti la hili jana kutoka Karatu mkoani Arusha, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba, alisema Kaze amepewa mkataba wa mwaka mmoja huku aliyekuwa Kocha Mkuu Denis Kitambi sasa atakuwa msaidizi wake na Shedrack Nsajigwa kuwa kocha wa viungo.

"Ni rasmi kaze amekuwa Kocha Mkuu Namungo FC kesho (leo) atakuja hapa Karatu tulipoweka kambi kuungana na sisi tunaomba wapenzi wa timu yetu tumpe ushirikiano," alisema Mkadeba.

Katibu huyo alisema Kaze amesaini mkataba wake huo jana jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuitumikia timu hiyo.

Alisema wamelazimika kumpa mkataba kocha huyo baada ya kuridhishwa na kazi yake na kudai ni miongoni mwa makocha bora nchini.

"Atatusaidia kuipa mafanikio timu yetu kwani ana historia nzuri ambayo tunaamini atatufikisha mbali zaidi msimu ujao unaotarajiwa kuanza ifikapoAgosti 15, mwaka huu," alisema.

Kwa sasa kikosi cha timu hiyo chenye maskani yake mkoani Lindi, kipo Karatu kwenye maandalizi ya msimu mpya wa mashindano 'pre season', ikipiga kambi yake na kufanya mazoezi kwenye Uwanja wa Black Rhino Academy.

Namungo kwa miaka ya hivi karibuni imekuwa ikibadilisha makocha mara kwa mara ambapo ilikuwa na Hanoor Janza raia wa Zambia akisaidiana na Jamhuri Kihwelo, hata hivyo hawamaliza msimu kabla ya nafasi hiyo kuchukuliwa na Kitambi ambaye kwa sasa anakwenda kuwa kocha msaidizi.

## Hilal aanza vizuri kuogelea dunia

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Kuogelea, Hilal Hemed Hilal, ameanza vema mashindano ya Dunia yanayoendelea nchini Japan baada ya kufanikiwa kushika nafasi ya kwanza kwenye kundi lake katika mbio za mita 50 (butterfly) kwa kutumia muda wa dakika 27.68.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka Japan, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Alexander Mwaipasi, alisema kwa muda aliutumia unafanya kuwa wa 74 kati ya washindi 89 kutoka makundi mengine.

Alisema amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na mchezaji huyo kwani ni mara yake ya kwanza kushiriki mashindano ya dunia.

"Hilal amefanya juhudi kwani mbio za aina hii hajawahi kushindana kwenye ngazi ya mashindano kidunia ikiwa ni pamoja na kutoshiriki kitaifa muda mrefu," alisema Mwaipasi.

Alisema endapo angefanya maandalizi mazuri nyumbani angepata matokeo mazuri zaidi ya hayo aliyoyapata juzi na kuwataka wachezaji wengine kuongeza bidii.

## BMT yataka medali michezo vyuo vikuu

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Vyuo Vikuu Tanzania, ambayo inatarajiwa kuelekea nchini China leo, Jumanne kwa ajili ya kushiriki mashindano ya vyuo vikuu yatakayoanza kutimua vumbi Julai 27 hadi Agosti 8, mwaka huu imetakiwa kupambana vema ili kuhakikisha inarudi na medali za ushindi nchini.

Tanzania itawakilishwa na Patrick James atakayeshiriki mchezo wa riadha pamoja na Naomi Amos anayekwenda kushiriki mchezo wa kuogelea.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati akiikabidhi bendera ya Taifa kwa timu hiyo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, aliwataka wachezaji hao kuhakikisha wanakwenda kuiwakilisha vema nchi yetu kwani wamebeba dhamana ya nchi kwa ujumla.

"Muende mkijua Watanzania tupo nyuma yenu, hivyo nendeni mkaitangaze Tanzania kupitia mashindano hayo na sisi tutaendelea kushirikiana na nyie," alisema Msitha.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**KANE KUPIGWA BEI SPURS**

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, ameambiwa lazima amuuze Harry Kane msimu huu wa majira ya joto ikiwa hawezi kumshawishi mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 29, kusaini mkataba mpya**. (Telegraph)**

**OLISE ATAKIWA CHELSEA**

CHELSEA wamewasilisha ofa kwa mchezaji wa Crystal Palace, Michael Olise, na winga huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 21, tayari ana makubaliano ya awali na 'The Blues' hao. **(RMC Sport)**

**CITY WAMTAKA OLISE**

KLABU ya Manchester City pia wanania ya kumsajili Michael Olise, ambaye ana kipengele katika mkataba wake cha kuuzwa kwa takriban pauni milioni 35. **(Fabrizio Romano)**

**MBAPPE AWANIWA AL-HILAL**

KLABU ya Al-Hilal itaweka dau la euro milioni 200 kwa ajili ya Kylian Mbappe wa Paris St-Germain na kumpa mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka mkataba wa miaka miwili wenye yenye thamani ya euro milioni 200 kwa mwaka. **(Tancredi Palmeri)**

**LUKAKU NA CHELSEA BADO**

CHELSEA wanachoshwa na kuishiwa uvumilivu na Romalu Lukaku, kutokana na mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 30, kugoma kuhamia Saudi Arabia na anasubiri klabu ya Ulaya kumsajili. **(Gazzetta dello Sport)**

**MBWA SHIDA KWA FABINHO**

Uhamisho wa Fabinho kutoka Liverpool kwenda Al-Ittihad uko hatarini kwani kiungo huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 29, anataka ufafanuzi iwapo anaweza kwenda na mbwa wake wawili huko Saudi Arabia. **(Express)**

**HOJLUND AWINDWA UNITED**

MSHAMBULIAJI wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20, anataka kukamilisha uhamisho wa kwenda Manchester United kufikia mwisho mwa mwezi huu akiwa tayari amekubali maslahi binafsi. **(TeamTalk)**

**ZAHA KUTUA GALATASARAY**

MSHAMBULIAJI wa Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 30, atajiunga na mabingwa wa Uturuki, Galatasaray baada ya kumaliza mkataba wake na Crystal Palace. **(Guardian)**

**SILVA AKATAA SAUDIA**

KOCHA Marco Silva amekataa ofa ya pauni milioni 40 kutoka kwa Klabu ya Al-Ahli ya Saudi Arabia na kuamua kubakia Fulham. **(Telegraph)**

**ZIYECH NAYE KUUZWA**

CHELSEA imeanzisha tena mazungumzo na timu za Saudi Arabia kuhusu kumuuza winga wa Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 30. **(Teamtalk)**

**ODOI KUJIUNGA NA SARRI**

WINGA wa England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 22, anakaribia kuungana tena na kocha wake wa zamani akiwa Chelsea, Maurizio Sarri kule Lazio. **(Gazzetta dello Sport)**

## DO A SOKA MAG A ULAYA



# MBAPPE SASA AGEUKA PASUA KICHWA PSG

●●●Anukia kuondoka bila malipo ikiwa klabu hiyo itashindwa kumuuza katika dirisha hili, lakini...

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa PSG, Nasser Al-Khelaifi, anafanya kila awezalo kumshawishi Kylian Mbappe kuondoka msimu huu wa majira ya joto' huku mshambuliaji huyo akitarajia uhamisho wa bure kwenda Real Madrid mwaka 2024.

Mustakabali wa Mbappe umeingia mashakani katika siku chache zilizopita, huku Mfaransa huyo akieleza kuwa atakataa kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo, wakati mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika msimu ujao.

Ana hatari ya kuondoka bila malipo ikiwa PSG hawataweza kumuuza katika dirisha hili la uhamisho. Mbappe ameachwa kwenye kikosi cha klabu hiyo kwa ajili ya ziara yake ya kujiandaa na msimu mpya nchini Japan, lakini anatamani kubakia klabuni hapo kwa muda wote wa mwaka huu kabla ya kuendelea na muhula ujao.

Hata hivyo, PSG wanatamani hilo lisitokee, huku Al-Khelaifi akikiri kwamba hawezi kuondoka bure. Na kulingana na Le Parisien, rais anashinikiza Mbappe kuondoka msimu huu wa majira ya joto.

Imeripotiwa kuwa PSG wanaweza kukubali ofa za chini ya pauni milioni 155 walizolipa kwa fowadi huyo katika jaribio la kutaka kumuondoa.

Klabu hiyo inaamini kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anatafuta kuhamia Real Madrid msimu ujao wa majira ya joto.

Mbappe amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na 'Los Blancos', lakini aliamua kusaini mkataba mpya na PSG badala ya kujiunga na timu hiyo ya Hispania.

Lakini mambo yamekuwa mabaya tangu wakati huo, Mfaransa huyo akinukuliwa mara kwa mara dhidi ya uongozi na kutishia kuondoka bure mkataba wake utakapomalizika.

Amekuwa akihusishwa na kuhamia Klabu za Arsenal, Chelsea na Ligi Kuu Saudi Arabia msimu huu wa majira ya joto, lakini dalili zote zinaonesha kuwa anataka kwenda Madrid.

Pia imependekezwa kuwa fowadi huyo anaweza kuwa tayari kukaa nje msimu mzima iwapo mabishano yataendelea.

Mbappe aliingia akitokea benchi na kufunga bao katika mechi ya kirafiki ya PSG dhidi ya La Havre Ijumaa, lakini baadaye aliachwa kwenye kikosi kilichosafiri kwenda kujiandaa na msimu mpya.

# LIVERPOOL KUSAJILI ZAIDI




**LIVERPOOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp amethibitisha kuwa Liverpool itasajili wachezaji zaidi msimu huu, huku Jordan Henderson na Fabinho wakijiandaa kuhamia Saudi Arabia.

Wekundu hao tayari wameimarisha kikosi chao kwa kumsajili Alexis Mac Allister kutoka Brighton kwa pauni milioni 35 na Dominik Szoboszlai kutoka RB Leipzig kwa pauni milioni 60.

Hata hivyo, dhoruba ya Saudia imehatarisha mipango yao kwani Jordan Henderson anakamilisha matibabu yake ya kujiunga Al-Ettifaq, huku Al-Ittihad na Bayern Munich zikimwinda Fabinho.

Msukosuko huo umewafanya kuhitaji kupanga safu ya kiungo ya kikosi cha kwanza endapo wataondoka na Klopp alithibitisha kuwa klabu hiyo bado haijakamilika katika soko la uhamisho.

"Kuna mambo mengi ya kufanya," alisema. Dirisha la uhamisho limefunguliwa. Ikiwa siku yangu ingekuwa na saa 28 kwa sasa haingekuwa shida - ningeweza kuzijaza kwa urahisi!

"Pamoja na mambo yote unayopaswa kufanya kushoto na kulia, lengo langu kuu na nguvu lazima niende kwenye vikao vya mafunzo basi ndivyo ninavyofanya. Kisha upande wowote wa vipindi naweza kujaribu kusaidia na mambo mengine.

"Bado wiki tatu na nusu kabla ya mchezo wa kwanza wa msimu. Mambo machache lazima yatokee kabla ya wakati huo, bila shaka.

"Hiyo ni wazi sasa. Na itatokea. Wachezaji wapya lazima waingie. Tutakuwa na timu nzuri."

# Son na uvumi wa usajili wa Kane

**LONDON, England**

MCHEZAJI Heung-Min Son, anahisi uvumi unaoendelea kuhusu Harry Kane "sio rahisi" kwa mchezaji mwenzake huyo, lakini amesifu weledi wa nahodha wa klabu hiyo.

Son na Kane wametua Singapore kwa awamu ya mwisho ya ziara yao ya awali ya kujiandaa na msimu mpya baada ya siku chache zenye matukio mengi mjini Bangkok nchini Thailand.

Hali ya hewa ilisababisha mechi ya kirafiki kati ya Tottenham na Leicester kufutiliwa mbali Jumapili na siku moja mapema mwandishi wa habari kutoka Jarida la Ujerumani, Bild, alizindua jezi ya Bayern Munich yenye 'Kane 9' mgongoni kwa kocha mkuu mpya wa Spurs, Ange Postecoglou katika mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mechi.

Postecoglou hakufurahishwa sana, lakini kelele za Kane hazioneshi dalili ya kuondoka, huku Bayern ikitarajiwa kurejea na ofa ya tatu baadaye mwezi huu.

Kane, ambaye anatekeleza majukumu ya unahodha wakati wa ziara ya Tottenham baada ya Hugo Lloris kuachwa England ili kukamilisha uhamisho wa kuihama klabu hiyo, amepongezwa na mshirika wake wa muda mrefu.

"Harry amekuwa mzuri kwangu," alisema Son akiwaambia waandishi wa habari huko Bangkok. "Yeye ni mtaalamu, daima anafanya kazi kwa bidii.

"Hajawahi kuonesha mawazo yoyote juu yake mwenyewe. Kuna habari nyingi sana pia si rahisi kwake, lakini ni nahodha kwa sasa na anafanya kazi na timu.

"Haoneshi usumbufu wowote. Anapenda kuwa hapa. Ninampenda kama mchezaji. Ninamheshimu kikamilifu.

"Yeye ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani, amekuwa kwa miaka mitano, sita, saba mfululizo. Uamuzi utakuwa kati ya klabu na Harry na tunapaswa kuuheshimu.

"Siwezi kusema chochote kuhusu uamuzi wa mwisho kwa sababu sijui chochote. Labda Harry hajui. Inabidi tusubiri tu."

Kane ameingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake pale Tottenham na Bayern wameongeza juhudi zao za kumsajili fowadi huyo mwezi huu, huku rais wao wa heshima Uli Hoeness akidai wiki iliyopita kuwa makubaliano binafsi yalikubaliwa kati ya klabu hiyo ya Ujerumani na nahodha huyo wa England.

Bayern wanaripotiwa kutuma maombi mawili ambayo hayakufanikiwa kwa Kane hadi sasa msimu huu wa majira ya joto, lakini Spurs bado wamedhamiria kumshikilia mfungaji wao huyo bora wa muda wote.

Mkataba mpya umetolewa kwa Kane na Tottenham, ambalo ni ongezeko kubwa katika mkataba wake wa sasa wa pauni 200,000 kwa wiki, lakini hajafanya uamuzi wowote kuhusu mkataba huo mpya huku uvumi juu ya mustakabali wake ukiendelea.

Spurs wanatarajiwa kucheza na timu ya ndani ya Lion City Sailors huko Singapore Jumatano kabla ya kurejea England.

# Onana atoa sababu kuchagua namba 24

**Manchester, ENGLAND**

ANDRE Onana ameeleza kwa nini amechagua kuvaa jezi namba 24 akiwa Manchester United, akisema aliichukua kwa sababu ni tarehe yake ya kuzaliwa.

Uhamisho wa Onana kwenda Man Utd ulithibitishwa rasmi Julai 20, mwaka huu huku mlinda mlango huyo akiweka bayana kuhusu mkataba wa miaka mitano - klabu hiyo ikisalia na chaguo kwa mwaka zaidi - baada ya 'Mashetani Wekundu' hao kukubali kulipa pauni milioni 47.61 kwa Inter kwa ajili ya huduma yake.

Huku David de Gea akiachana na jezi namba moja baada ya kumalizika kwa mkataba wake pale Old Trafford, Onana alitarajiwa kurithi namba moja, cha kushangaza ni kwamba Mcameroon huyo badala yake aliamua kuchagua namba 24.

Akielezea uamuzi huo kwa MUTV, Onana alisema: "Naipenda hiyo namba. Ni siku yangu ya kuzaliwa. Tarehe yangu ya kuzaliwa. Kwangu ni nzuri, ni nzuri.

"Ninapenda jezi hii kwa sababu namba hii tumefanya mengi na natumaini itaendelea."

Onana alivaa jezi namba 24 wakati alipokuwa Inter, huku Samir Handanovic akiwa na jezi namba moja, na pia aliivaa Ajax pia.

Onana alivaa jezi hiyo alipowasili klabuni hapo kwa mara ya kwanza na, kufuatia msimu mmoja usiopendeza akivaa nambari moja msimu wa 2017/18, alirejea kwenye namba yake ya jezi aliyoipenda zaidi kampeni iliyofuata.

Katika mahojiano yake ya kwanza pale Manchester United, Onana pia alijadili mtindo wake wa uchezaji na hisia zake za kwanza za mazoezi na wachezaji wenzake wapya.

"Nina raha sana. Nadhani jambo muhimu zaidi ni kutambua hali hiyo na ndivyo ninavyofanya mwenyewe, kusoma hali, haswa kile timu inahitaji katika wakati fulani.

"Tunapocheza kutegemea tunacheza na nani, wakati mwingine unamiliki mpira na wakati mwingine huna, hivyo kutoka hapo lazima uwe na akili na ujaribu kusaidia timu, kwa sababu muda mwingi kucheza na hawa wachezaji ni jambo la kushangaza.

"Nilikuwa na kikao changu cha kwanza cha mazoezi nao na inashangaza ubora wa hapa, ni mzuri."

HABARI MICHEZO

# NYOTA SIMBA WAMSUBIRI MIQUISSONE KWA HAMU

**Na Faustine Feliciane**

SIKU chache tu baada ya uongozi wa Simba kutangaza kumsajili tena winga Luis Miquissone, aliyevunja mkataba na klabu yake ya Al Ahly ya Misri, baadhi ya wachezaji waliopo katika kambi ya timu hiyo nchini Uturuki wameelezea kuvutiwa na ujio wa nyota huyo na wanamsubiri kwa hamu kubwa kuungana naye tena.

Jumamosi Simba ilitangaza kukamilisha usajili wa Miquissone kwa mkataba wa miaka miwili na sasa anajiandaa kwenda kuungana na wachezaji wenzake kwenye kambi ya timu hiyo nchini Uturuki.

Kiungo wa timu hiyo, Clatous Chama, aliliambia Nipashe kuwa kwake ni furaha kuungana na nyota huyo na anaamini ataongeza kitu kwenye kikosi chao kilichopania kurejesha makombe waliyoyapoteza misimu miwili mfululizo.

Chama alisema wanafahamu ubora wa Miquissone na wanaamini ataleta kitu kingine ndani ya timu hiyo kwa msimu ujao.

"Ni moja ya usajili tulioufurahia kaka..., wengi tunajua uwezo wake, kuja kwake na usajili mwingine uliofanyika tunaamini msimu ujao tutakuwa wa moto, tunamsubiri 'Konde Boy' tuungane naye tena," alisema Chama.

Aidha, Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Mohamed Hussein 'Tshabalala' alisema kwa namna anavyokiona kikosi cha timu hiyo ana uhakika wa kufanya vizuri msimu ujao.

Alisema wamepata taarifa ya kusajiliwa kwa Miquissone na wachezaji wamefurahia kurejea kwake tena kwenye kikosi cha timu hiyo.

Kwa mujibu wa msemaji wa klabu hiyo, Ahmed Ally, Miquissone atajiunga na wachezaji wenzake nchini Uturuki muda wowote kuanzia sasa tayari kwa maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa.

Miquissone aliuzwa na Simba mwaka 2021 kwenda Al Ahly baada ya kuonyesha uwezo mkubwa alipojiunga na Wekundu wa Msimbazi hao akitokea UD Songo ya Msumbiji aliyokuwa akichezea kwa mkopo akitokea Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.




Miquissone

# Mandonga afurahia kutopigwa kwa KO

**Na Abdallah Mataka**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, mwenye mbwembwe na tambo nyingi, Karim Mandonga, amesema amefurahia matokeo ya pambano lake mwishoni mwa wiki hii dhidi ya Daniel Wanyonyi kutoka Kenya licha ya kwamba alichezea kichapo.

Akizungumza na Nipashe baada ya pambano hilo, Mandonga alisema haikuwa siku nzuri kwake na bahati ilimwangukia Wanyonyi lakini hakukosea kwa sababu hakupigwa kwa KO (Knockout).

"Siku ya leo [Jumamosi], naona ilikuwa bahati yake, lakini hakuna kitu ambacho nimekosea kama nimekosea angenipiga kwa KO(knockout), mimi nilimpiga yule kwa KO," alisema.

Mandonga aliongeza kuwa hakuna alichokosea huku akisema kuwa mchezo ndivyo ulivyo ukimaliza kuna matokeo matatu ambayo ni suluhu, kushinda au kushindwa kwa hiyo amekubaliana na matokeo.

Katika pambano hilo la raundi 10 uzani wa Light Heavyweight, lililofanyika jijini Nairobi, Kenya Jumamosi usiku, majaji wote watatu walimpa Wanyonyi ushindi.

Jaji George Athumani alimpa Wanyonyi alama 100-80, Waycliffe Marende akampa 100-80 na Leonard Wanga 100-89.

Hilo lilikuwa ni pambano la pili kwa mabondia hao wa Afrika Mashariki kukutana, katika pambano la kwanza lililofanyika Januari huko huko Nairobi, Mandonga alimchapa Wanyonyi kwa TKO (Technical Knockout).

Wakati huo huo Mandonga anatarajia kupanda tena ulingoni Jumamosi wiki hii kuzichapa dhidi ya Moses Golola kwenye 'Usiku wa Vitasa' unaotarajiwa kufanyika jijini Mwanza.

## Kibu aipa Simba sare Uturuki, Sakho auzwa

INATOKA UK. 24

kirafiki jana, Moses Phiri kama angekuwa makini, angeweza kuiandikia Simba bao dakika ya 18 alipogongeana vema na Willy Onana na kisha dakika ya 43, kushindwa kutumia pande murua kutoka kwa Saido Ntibazonkiza.

Bao la Simba lilifungwa dakika ya 33 na Kibu Denis ambaye alimalizika kazi nzuri iliyofanywa na Saido kabla ya kuukwamisha wavuni kwa shuti kali, likidumu hadi mapumziko.

Kipindi cha pili Phiri alitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Aubin Kramo na dakika ya 58, Zira FC walifanya mabadiliko ya wachezaji wanane kwa mpigo.

Zira FC ilisawazisha bao dakika ya 64 kupitia kwa Rustam Ahmadzada, akiyatumia vema makosa ya mlinzi Kennedy Juma aliyeingia kipindi cha pili, na ni dakika ambayo alitoka Onana na kuingia Clatous Chama kabla ya dakika ya 75, Kramo kumpisha John Bocco.

Kiungo huyo mshambuliaji alikosa bao la wazi dakika ya 70, baada ya kazi safi iliyofanywa na John Bocco, huku Kibu naye akikosa bao la wazi dakika nane kabla ya mechi kumalizika.

Dakika tatu kabla ya mechi kumalizika, Fabrice Ngoma aliingia kuchukua nafasi ya Kibu na Sadio Kanoute alimpisha Israel Mwenda.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, timu hiyo itakuwa na mechi zingine mbili ikiwa nchini humo kabla ya kurejea nchini Julai 2, mwaka huu tayari kwa maandalizi ya Tamasha la Simba Day na Ngao ya Jamii.

Kuhusu kuuzwa kwa Sakho, kwa mujibu wa taarifa ya Simba iliyotolewa jana mchana, wamefikia makubaliano ya pande mbili pamoja na mchezaji huyo kumuuza kwa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Daraja la Pili chini Ufaransa baada ya kiungo huyo raia wa Senegal kuitumikia kwa misimu misimu miwili.

"Simba tumefikia makubaliano na Klabu ya Quevilly Rouen Metropole (QRM) ya nchini Ufaransa kumnunua mchezaji wetu Pape Sakho," ilieleza taarifa hiyo katika mtandao wa instagram wa klabu hiyo.

Taarifa za ndani kutoka katika klabu hiyo, zinadai Sakho ambaye bado alikuwa na mkataba wa mwaka mmoja, ameuzwa kwa dau lisilopungua Sh. billioni mbili za Tanzania.

Quevilly Rouen Metropole inashiriki League 2 ambayo hapa nchini ni kama Ligi ya Championship, msimu uliomalizika ilimaliza nafasi ya 11 na pointi zake 50 katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

## Gamondi aahidi Yanga yakutisha

INATOKA UK. 24

kayoshiriki.

Kikosi hicho cha Yanga kuinaendelea na maandalizi yake kwenye kambi waliyoiweka Avic Town Kigamboni kujiandaa na michezo ya Ngao ya Jamii na Ligi Kuu kwa ujumla wake.

Kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii, Yanga itafungua pazia dhidi ya Azam FC Agosti 9, huku Simba wakicheza na Singida Fountain Gate FC Agosti 13 mwaka huu.

Michezo
Jumanne Julai 25, 2023
Nipashe



## Mbappe ageuka pasua kichwa PSG

UKURASA 21

# KIBU AIPA SIMBA SARE UTURUKI, SAKHO AUZWA

●●●Apiga bao kali dhidi ya wakali wa UEFA Europa Conference League, Sakho aiingizia mkwanja mrefu...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikitangaza kumuuza rasmi kiungo mshambuliaji wao, Pape Sakho, kwa Klabu ya Quevilly-Rouen Metropole (QRM) ya nchini Ufaransa, jana miamba hiyo ya Tanzania imetoka sare ya bao 1-1 katika mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Zira FC ya Azerbaijani, mechi ikipigwa nchini Uturuki.

Simba ambayo ipo nchini Uturuki kwa maandalizi ya msimu ujao wa mashindano, ilicheza mechi hiyo mbele ya Kocha Mkuu, Robertinho Oliveira, ambaye alikuwa amerejea kambini kutoka kwenye kozi fupi nchini Brazil.

Timu hiyo ilichezesha wachezaji wa zamani na wGamondi bao wamesajiliwa msimu huu, huku wengine na haswa waliokwenda Uturuki awamu ya nne wakiwa watazamaji.

Dakika ya 20, kipa Ally Salim alifanya kazi ya ziada kwa kuokoa penalti ambayo wapinzani wao walipata, ikipigwa na Filipe Patchmann.

Zira FC ni timu inayocheza Ligi Kuu nchini Azerbaijani na msimu ulioisha wa 2022/23 ilishiriki michuano ya UEFA Europa Conference League, na yenyewe ipo nchini Uturuki ikijiandaa na msimu mpya baada ya uliomalizika kumaliza nafasi ya tano kwenye ligi yao.

Katika mchezo huo wa

UKURASA. 23



Pape Sakho akiwa na uzi wa klabu yake mpya, Quevilly-Rouen Metropole (QRM), baada ya jana kukamilisha usajili wa kujiunga na miamba hiyo ya Ligi Daraja la Pili nchini Ufaransa. **PICHA: MTANDAO**

## Gamondi aahidi Yanga yakutisha

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amewataka mashabiki wa klabu hiyo kutarajia mabadiliko zaidi ya uchezaji kwa timu yake tofauti na walivyoishuhudia kwenye mchezo wao wa kirafiki dhidi ya Kaizer Chiefs katika Tamasha la Kilele cha Siku ya Mwananchi Jumamosi.

Akizungumza na mwandishi wetu, Gamondi alisema anahitaji marekebisho madogo kwenye timu yake na anaamini timu hiyo itaendeleza makali yake kwenye ligi na mashindano ya kimataifa.

"Mashabiki wa Yanga wataendelea kufurahi, naamini kikosi hiki kitafanya vizuri kwenye mashindano yote, yapo marekebisho kidogo nitayafanya mazoezini na timu itakapoonekana kwa mara nyingine mashabiki wataona mabadiliko, nina wachezaji wenye uwezo mkubwa sana," alisema Gamondi.

Alisema siku zilizobaki kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu kuanza hapo Agosti 15, mwaka huu, atazitumia vizuri kuweka kile anachokitaka ndani ya timu hiyo na kuwataka mashabiki kujiandaa kupata furaha.

Alipoulizwa ni mapungufu gani aliyoyaona ndani ya timu hiyo, Gamondi hakutaka kuweka wazi lakini alisisitiza lazima wachezaji wake watengeneze nafasi nyingi za kufunga na wazitumie ipasavyo.

"Siwezi kusema, lakini kama kocha nina ramani yangu kichwani ya namna timu ninavyotaka icheze... ni lazima tutumie vizuri kila nafasi tunayoitengeneza, kwa sasa bado timu haijakaa vizuri kwa namna ninavyotaka," alisema Gamondi.

Aidha, alisema ameguswa na uwezo wa wachezaji wake na ana uhakika watampa matokeo mazuri kwenye mashindano wata-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >